

## ELIMUNAFSIA-JINSIA

### MALEZI YANAYOHITAJIKA

Nchi za Afrika zilipojikomboa **zilikazania elimu** ili kupata mapema wataalamu kwa kazi na huduma za jamii. Hasa siku hizi wengi wameona umuhimu wa kusoma ili kukabili maisha. Ila mara nyingi juhudhi hizo hazilengi kujua ukweli, bali kufanikiwa katika kazi na uchumi, na **zinaweka pembedi maadili** yaliyokuwa muhimu katika malezi ya kimila. Hayo yalikusudiwa kuwaandaa watoto na vijana kwa maisha, wawe washiriki wa ukoo na kabilo ambao wamekomaa kiasi cha kuweza kuchukua majukumu yao. Hata leo bila ya hayo ujuzi na ufundi vinawenza kuongezeka, lakini **ukomavu haufikiwi**. Hivyo vijana wanachelewa kushika nafasi yao katika ujenzi wa jamii, k.mf. kwa njia ya ndoa. Badala yake unaenea uhuni (uasherati, bangi, wizi n.k.).

Kwa kuwa ujana ni kipindi cha mabadiliko ya haraka pande zote, ni vigumu kuumudu sawasawa na **kuwa na msimamo**. Hasa mijini kuna mchanganyiko wa watu (makabila, dini n.k.) pamoja na njia hasi za kuishi zinazotokana na ushindani mkubwa, utepetevu katika maadili na upotovu. Katika hali hiyo **dini ya ukoo si kinga tena**: kijana mwenyewe anajichagulia aamini nini na aishi vipi badala ya kufuata tu mazoea ya nyumbani kama alivyofanya utotoni. Anahitaji kusaidiwa ajibu **maswali makuu ya maisha**: "Mimi ni nani? Nitemoka wapi? Ninakwenda wapi? Nafikiriwa kuwa wa namna gani?" Kumbe watu wazima wengi wanamsema badala ya **kujihusisha naye katika matatizo yasiyoepukika ya umri wake**. Anahitaji kueleweka na kuthaminiwa, lakini akitafuta hayo anaitwa jeuri, mwenye kiburi n.k.

Hasa siku hizi kati ya wazee na vijana **umbali ni mkubwa** kutokana na mabadiliko ya nyakati (upande wa elimu, afya, uchumi, mawasiliano, tunu za maisha n.k.). Vijana wanaonelea miundo asili ni mambo ya zamani, hata **wakadharau utamaduni wa mababu** kama kwamba mambo yake yote yamepitwa na wakati. Kinyume chake wanapokea kwa urahisi mkubwa mawazo mengi ya kigeni kupitia vyombo vyaya upashanaji habari na mitindo mipyi inayozuka mijini. Halafu wanatumia muda mwingu kijiweni au katika burudani, kumbe ule wa **kukaa na wazee** ni mfupi mno: hilo ni pengo lisilozibika, kwa kuwa linawafanya wakose kufaidi mang'amuza ya vizazi vilivytangulia, kutegemezwa na mashauri wanayoyahitaji, kuungana na ndugu zao katika kukabili maisha. Wanakuwa **jamii tofauti**, wageni kati ya watu wao! Wazee wengi wanaona vijana wakiungana ni nafasi tu ya kujenga urafiki mbaya, si **haja halisi** ya nafsi na ya maisha. Hivyo badala ya **kuwasaidia kuchambua mambo** wanazidisha hali ya kutoelewana nao.

Basi, hatuna budi **kulea kwa kuoanisha ujuzi na ukomavu** ili tupate watu tunaowahitaji kadiri ya mpango wa Mungu: watu ambao ni huru kwa ndani na wanaweza kuwajibika kwa uadilifu. Hata malezi ya kitawa yasiishie kufundisha Biblia, katekisimu, liturujia, maisha ya Kiroho n.k. Ni muhimu vilevile kuhakikisha kijana anazidi **kukomaa kiutu**. Kwa ajili hiyo anahitaji **kusaidiwa ajifahamu** ili kustawisha vipawa vyake na kupunguza kasoro zake. **Utu ndio msingi** ambao juu yake yanajengwa maisha yote, hata utume. Kabla ya kuwa Mkristo na mtawa kila mmoja ni mtu. Mwenye **matatizo nafsini** mwake anasumbuka na kusumbua watu anaofungamana nao. Basi, ni muhimu **awahi kujirekebisha** kama inavyobidi kuwahi ili kunyosha mti ukiwa bado mbichi. Ni lazima aifanyie kazi nafsi yake kwa **ustadi na bidii** nyingi kuliko mkulima anavyoshughulikia shamba lake ili lizae sana.

### HADHI YA BINADAMU

Binadamu ameumbwa kwa mfano wa Mungu, mwenye roho isiyokufa. Ameshirikishwa naye ukuu juu ya viumbe vyote inavyoonekana. Yeye tu ni nafsi, anaweza kujifahamu, kujitawala, kujitolea na kupendana na wengine. Basi, anapaswa **kulinda hadhi** hiyo asitawaliwe na tamaa za kila aina. Akifanya hivyo anatimiza mpango wa Mungu juu yake na kupendana naye. Utotoni anasukumwa tu na haja za umbile lake, ambazo ni **muhimu kwake** na anazilenga bila ya kuhitaji juhudhi. Lakini akikua anaanza kutambua **tunu za maadili na dini**, ambazo ni njema, ni **muhimu kwa zenyewe** na zinamda azifuate kwa nia imara hadi afikie lengo. Kwa **bidi za kudumu** za namna hiyo **anamlenga hasa Mungu**, wema mkuu. Anapopitia misukosuko ya ujana asikubali kushindwa na vionjo wala asikate tamaa, kwa kuwa Mungu amemuumba **atawale** hata nafsi yake na mwili wake. "Mungu aliona kila kitu alichokifanya, na tazama ni **chema sana**" (Mwa 1:31). Hata hivyo, baada ya **dhambi ya asili** tunadaiwa bidii katika kutekeleza tunu ili wema tulionao uzae matunda. Basi, tupanie kukuza wema tuliojaliwa ili kesho tuwe **watu bora** kama wazazi, raia, watawa, viongozi wa Kanisa na jamii n.k. Penye nia **pana njia** hata ya kuelekea utakatifu utakaokamilika katika uzima wa milele.

Tumekabidhiwa na Mungu dunia, lakini **hasa tumekabidhiwa nafsi yetu** wenye. Itatufaa nini kujua na kutawala ulimwengu, tusipojija na kujitawala kweli? Kwa maongozi ya Mungu karne XX imeleta **maendeleo makubwa katika elimunafsia** (= saikolojia). Hivyo tunaweza kutambua vizuri mema na mabaya yaliyomo ndani mwetu. Lakini tukitaka kujifahamu haitoshi tusikilize mafundisho hayo au kusoma vitabu vingi juu yake. Tunahitaji kuishi katika **mazingira bora** ambapo tujisikie nyumbani, huru na watulivu kwa kupendana na wenzetu, **kusikiliza watu** wanaotufahamu (hasa walezi wetu) wanamsema nini juu yetu, kujipatia muda wa **kutulia peke yetu** na kujifikiria kulingana na maneno yao, **kujichunguza kwa makini kuanzia miaka ya utotoni**. Kwa kuwa **utu unategemea urithi, mazingira na utashi wa kila mmoja**, tunapaswa kuchunguza hayo yote yaliyochangia kutujenga. Mara kwa mara tujitenge na watu na shughuli ili kutathmini tena maisha

yetu, kupima maono yetu na kuweka maazimio ya kufaa, bila ya kusahau kwamba uhai wetu ni fumbo, kwa kuwa unamtegemea Mungu.

## KUJIFAHAMU

Hakuna mtu wa jana, leo au kesho aliye sawasawa na mwengine: **kila mmoja ni wa pekee**. Mungu ametufanya tofauti ili **tutimilizane**. Kila mmoja anahitaji wengine, na kila mmoja ni muhimu kwa wenzake. Katika maisha kuna sehemu ambayo yeye tu anaweza kujaza. Wazo hilo linawenza kumsaidia kijana ambaye ni mwepesi kukata tamaa na kujitupa. Daima **uhai ni zawadi** nzuri ya Mungu kwa mhusika na kwa wenzake wote. Kijana ni zawadi yenyenye **nguvu na wema** hata kwa taifa na Kanisa, kiasi kwamba **kujali ustawi wa kijana** ni kujenga taifa na Kanisa.

Tunataka kujifahamu tulivyoumbwa (**mwili, nafsi na roho**, ambavyo vyote vinafungamana ndani mwetu):

1. ili tuweze **kujithamini** hasa kwa kuona sisi ni nani mbele ya Mungu;
2. ili tufahamu **mipaka** yetu na kuikabili inavyofaa;
3. ili tufahamu **vipawa** tulivyojaliwa tuwashirikishe wenzetu;
4. ili tubadilike **kuwa bora zaidi** na kuchangia ustawi wa jamii;
5. ili **tuhusiane vizuri** zaidi na wenzetu;
6. ili tuweze **kujieleza** kwa watu fulanifulani na kupata mashauri ya kutufaa.
- 7.

## KUJIKUBALI

Daima ni muhimu tukubali hali ilivyo, halafu tujitahidi kuifanya bora zaidi. Tusipojikubali kwanza tutahangaika tu hata kukata tamaa. Wajue wasijue vijana wapokua **wanashindwa kujikubali** walivyo. Pengine **wanaficha tabia zao** wasitambulikane na watu, hata wakashindwa kujielewa, wakapatwa na vilema vya ukuaji pia. Ni lazima waache kujifunika uso kwa vinyago hivyo; badala yake **wakabili ukweli wao**, wenye sifa na kasoro. Hivyo tu watapitia vizuri mabadiliko ya ujana upande wa mwili, nafsi, jamii, maadili na roho. Hatimaye watakoma na kushika nafasi yao maishani.

Kwa kila mtu ni muhimu **kuwa na marafiki**; hasa kijana anahitaji kikundi. Lakini hiyo isiwe njia ya kukwepa nafsi yake mwenyewe wala ya kuficha tabia yake kwa kuzungumza, kutembea au kutenda namna fulani wanavyofanya wenzake. Kwa hiyo **asijifananishe** nao. Kila mtu anakua kwa namna yake, akibadilika kwa kiasi tofauti na muda tofauti. Ni lazima ajifunze **kuyapokea mabadiliko hayo** pia yanayomfanya **geugeu sana, hasa wasichana** katika mzunguko wao wa kila mwezi: mara wanaonekana jasiri au korofi, mara wamejea wasiwasi.

## KUJISTAWISHA

**Uhai unasukuma kiumbe chochote kistawi.** Mimea inakua namna yake, wanyama namna yao, na binadamu **polepole** zaidi kwa kuwa ndiye kiumbe bora anayehitaji **kukomaa pande zake zote**. Kulingana na haja yetu ya kukomaa hivyo, **sio tu kufikia umri au kimo fulani**, ndani mwetu zimo nguvu zinazotuhimiza tujilinde ili tuzidi kuishi wenyewe, tuendeleze uhai tulionao kwa kuzaa, tujitegemee (yaani tumiliki maisha yetu), tutawale vitu na watu ili mambo yaende tunavyotaka, n.k.

Haja iliyoota mizizi mirefu ndani mwetu ni ile ya **kujikamilisha** tusiwe watu wanaoishi ili mradi tu. Kadiri tunavyokua tunajisikia kuwajibika. Haja hizo zinafanya **tujiwekee pia malengo** katika utendaji. Basi, baada ya kujifahamu, kila mmoja wetu achague na kuazimia awe bora vipi, kwa sababu wenyewe **tunaamua tuweje**. Ni **wajibu wetu kujipenda** na kwa hiyo kujitunza na kujistawisha kimwili, kinafsi, kijamii, kimaadili na kiroho. Kazi hiyo inahitaji nia na bidii za kudumu. Tufuate taratibu za kulinda **afya ya mwili, heshima ya mavazi, usafi wa mazingira**. Tujiepusha na **uvivu** unaosababisha mawazo na matendo mabaya. Tujihadhari na maandishi, picha na maneno **yasiyofaa**, yasije yakatupotosha kimawazo au kusisimua vionjo vya tamaa mbaya. Tuhusiane vema na wengine (adabu, lugha nzuri n.k.). Hasa tufuate dhamiri na kustawisha **roho iliyo sehemu bora** ya utu wetu ambamo tunashirikiana na Mungu.

Mbali ya **motisha kutoka nje** (yaani kupewa tuzo au adhabu), sisi binadamu tuna **maarubu yanayotuongoza kwa ndani** na kututia nguvu tutende namna fulani na kukwepa mambo mengine. Yanawenza kuwa ya aina mbalimbali:

1. **tusiyofundishwa** kwa kuwa ni haja za mwili (kupumua, kunywa, kula, kujisaidia, kupumzika, kutumia jinsia n.k.) au za nafsi (kupendwa, kufungamana, kukubaliwa, kufanikiwa, kujitokeza, kusaidia, kushindana, kushinda, kutawala, kujihami, kuwa salama, kuongozwa, kujishusha, kujitawala, kumiliki, kupanga, kubadili, kujua, kuhemka, kujamiihana, kucheza);

2. **yaliyorithiwa** kwa wazazi na ukoo (silika, maelekeo, vipawa n.k.);

3. **ya kujipatia**, yaani tusiyozaliwa nayo, ambayo tunayapata maishani mwetu hasa kutoka kwa watu wanaotuzunguka (mazoea, mila, tunu, imani n.k.).

Maarubu hayo yanasaidia kukua na kuelekea ukomavu, yaani hali ya **kuwa jinsi Muumba alivyokusudia kisha kupitia hatua kadhaa**.

## UKUAJI WA MTU NAFSINI MWAKE

Ukuaji wa mtu ni safari ya kutoka utotoni kuelekea utu uzima. Unadai tujipokee tulivyo, pamoja na mema na mapungufu yetu, tukimshukuru Mungu kwamba anatupenda tulivyo. Lakini ni lazima pia tupambane na mapungufu yetu ili kustawisha mema tulioyjaliwa. Kukua kiutu kweli ni kuwajibika maishani kadiri ya mpango wa Mungu aliyetumba. Safari hiyo ina **hatua mbalimbali, ambazo kila mojawapo ina kazi yake maalumu na ugumu wake**. Kazi hiyo ifanyike katika mazingira ya kufaa, la sivyo tutadumaa.

## HATUA NANE ZA UKUAJI KADIRI YA ERIKSON

1. Mtoto mchanga (miaka 0-2)
2. Mtoto aliyeachishwa (2-4)
3. Chekechea (4-7)
4. Mwanafunzi wa shule ya msingi (7-13)
5. Kijana (13-20)
6. Mtu mzima (20-35)
7. Mtu wa makamo (35-60)
8. Mzee (60 n.k.)

**Hatua za kwanza ni fupi lakini muhimu** sana, kwa sababu mambo yanayotokea wakati huo **yanaathiri maisha yote**. Mtoto akisaidiwa vizuri atakuwa mtu ambaye anajisikia salama, anaona mazingira kwa utulivu, anajitawala, anajiamini, haogopi kuwajibika na kuanzisha mambo.

Katika hatua nne za kwanza mtu anahitaji **kuziba mapengo** yake, katika zile nne za mwisho anahitaji **kustawi**.

Katika kila hatua hana budi **kufanya kazi fulani na kukabili ugumu** maalumu ili **kukua**. Vilevile anahitaji kusaidiwa kufanya hivyo (ndiyo **malezi**). Tunapitia **hatua hizohizo kila tunapoingia maisha mapya** (k.mf. utawani).

### 1. KUJIAMINI NA KUAMINI WENGINE

Mtoto anapozaliwa anaanza kuishi katika **ulimwengu tofauti** na ule aliouzoea tumboni mwa mama. Yuko kwenye hewa na mwanga badala ya kuogelea katika majimaji. Anapaswa kupumua na kutafuta mahitaji yake **mwenyewe**, ingawa bado anamtegemea sana mama (kwa maziwa, upendo, usalama n.k.).

Ugumu wa kipindi hicho ni kwamba anataka kuwa naye daima, lakini wao **ni watu wawili tofauti**. Hivyo anapaswa kukubali ukweli huo na kuanza **kujiamini**.

**Anaanza kutambua kama anapendwa** na kupokewa au la, naye anaanza **kutofautisha watu** wa kuwaamini na wale ambao asiwaamini.

Anahitaji **upendo, usalama** na chakula toka kwa mama.

### 2. KUJITAWALA NA KUONGOZWA

Mtoto wa miaka 2-4 anatembea, anasema, **anacheza na kuvumbua** vitu vingi, anaanza kujitambua na kutambua uhusiano wake na ndugu. Anaanza kutumia utashi ili **kujitawala**: miaka hiyo anasema mara nydingi, **"hapana"** na kugongana na mzazi.

Ugumu ni kufaulu kujitawala; akishindwa atakuwa daima na **aibu na shaka**, hasa akilaumiwa na kupewa adhabu kali mno.

Anahitaji kupokewa na kusaidiwa akuze mema anayoyafanya. Anahitaji pia **unyofu** na msimamo wa **nidhamu** kutoka kwa wazazi. Ikiwezekana **wamueleze** kwa ufupi lakini wazi sababu za kumkataza. Pengine anahitaji kuvumiliwa.

### 3. KUANZISHA MAMBO

Mtoto wa miaka 4-7 anawaza sana kwa **ubunifu**. Ndio wakati wa **kuuliza maswali** mengi, "Kwa nini...?". **Anafyonza na kuiga** lolote lile. Anaanza kutambua tofauti za jinsia, na mwenendo unaomfaa kama mtoto wa kiume au wa kike.

Ugumu ni kwamba asipojibiwa maswali atajisikia kutupwa. Hivyo ni rahisi kuwa **atajisikia daima na hatia**, hata asipofanya kosa.

Anahitaji kupokewa, kukubaliwa, kujibowiwa.

### 4. KUTENDA

Mtoto wa miaka 7-13 anachukua **majukumu ya kiadili**. Kisha kutofautisha uadilifu na uovu, anachagua kutenda mema au mabaya. **Anapanua mawazo**, anafanya kazi za mikono, **anatengeneza vitu**. Pia anajenga **uhusiano na wengine**, anafanya kazi pamoja nao. Anahisi kuwa anaweza au hawezo. Ni umri mzuri wa

**kufundishwa dini** na kuongozwa kiadili. Kwa kuwa ana mambo mengi ya kufanya, **jinsia huwa imelala**, kabla haijamka katika ubalehe. Lakini hiyo inategemea mazingira na malezi.

Ugumu ni kwamba asiposaidiwa sawasawa **atakuwa mnyonge** daima, atajiona hawezo chochote, au walau si sawa na wengine. Hivyo mazingira yanaweza kumjenga au kumbomoa.

Anahitaji kutiwa moyo (anapenda ukweli na sifa) **ajihisi anawenza** kufanya kitu, atambue mahitaji ya wengine na kuwasaidia wayapate.

## 5. KUJIPATIA TASWIRA-NAFSI

Umri wa miaka 13-20 ni kipindi cha **mpito** chenye **mabadiliko mengi yanayoathiri mwendo mzima** wa kijana ili atoke utoto na kuingia utu uzima. Msichana **anabalehe** mapema kuliko mvulana. Mvulana ana mwamko mkubwa kuliko msichana. Kuna **mvuto mkubwa** kati yao, hivyo wanahitaji **kuongozwa na nidhamu** safi (maadili ya unyago). Ni kipindi cha vurugu na cha **hisi kali** (kulia, kucheka n.k.). Akili inapanuka sana na kupenda nadharia; hivyo ni wakati wa **kujipatia maarifa**.

Ugumu ni kwamba **hatambui mahitaji yake halisi** (yuko wapi, naye ni nani?), **anaogopa** (je, atafaulu kuwa mtu mzima?), **hajui kutumia hiari** yake vizuri, anataka kuishi **tofauti na maelekezo** ya wazazi ili ajitegemee. Kutokana na hayo anayatilia **shaka** mafundisho ya dini (ukweli uko wapi?).

Anahitaji kujifahamu na kujipatia msimamo (**taswira-nafsi**) katika maisha, la sivyo atazama katika vurugu tupu.

## 6. KUFUNGAMANA NA WATU

Kati ya miaka 20 na 35 kijana anakuwa mtu mzima na kuweza kufungamana kwa dhati na wengine kwa **kupenda na kupendwa**, na kwa **kushirikishana** yaliyo muhimu. Hiyo inatakiwa sio tu katika ndoa, bali hata utawani ili mtu aishi kulingana na umri wake.

Ugumu ni kutojifahamu na kuogopa kufahamika alivyo.

Anahitaji kuvumilia, kuheshimiana na watu pamoja na kujali mipaka katika kupendana.

## 7. KUZAA MATUNDA

Kati ya miaka 35 na 60 mtu anapaswa kuzaa matunda, kuonyesha matokeo ya maisha yake, hasa kwa **kulea wanaofuata na kwa kuwatunza waliotangulia**.

Ndio ugumu wake; asipofanya hivyo mtu anabaki tasa.

Anahitaji **kukubali uongozi na kujitolea** zaidi na zaidi.

## 8. KUJUMLISHA MAISHA

Baada ya miaka 60 mtu anatakiwa **kukusanya vipande** vya maisha yaliyopita na kuleta **umoja** katika nafsi yake.

Ugumu ni kwamba hataki kuzeeka, kumbe **anapoelekea kifo** sharti aendelee kuzaa matunda kwa **kushirikisha hekima** ambayo alijipatia na ambayo inatarajiwa kumuandaa kwa kifo.

Anahitaji kuyapoea maisha yalivyo sasa, pamoja na **mipaka inayozidi** kutokana na uzee (hadi ukongwe). Asiporidhika atakata tamaa, na kuanza **kunung'unika**, kulaumu na kupatwa na wasiwasi kila mara.

## SIFA ZA MTU ALIYEKOMAA

1. **Anayatambua mambo yalivyo.** Anajitambua na kuwatambua wengine walivyo. Anatambua matukio pia katika sifa na kasoro. Anatambua yale anayoyaweza na yale asiyoyaweza. Hana wivu wale hofu. Anapima hali mbalimbali bila ya kufumba macho mbele ya mambo yasiyompendeza bali anatumia akili akabiliane nayo.

2. **Anakubali hali ilivyo.** Anajikubali na kuwakubali wengine walivyo. Akiona kasoro hachukii, bali kwanza anakubali hali ilivyo, halafu anajitahidi kuirekebisha iwezekanavyo. Hata akishindwa anakubali na kuvumilia. Vilevile anaweza kuyakubali mabadiliko na mambo mapya bila ya hofu, kwa kuwa anapima yote bila ya kufadhaika kwa kusema, "Itakuwaje?".

3. **Anawajibika.** Hangoji kuambiwa kila mara afanye nini na vipi, bali anaona mwenyewe anavyotakiwa kutenda, halafu anaamua kwa moyo ayatende. **Ndiyo sifa kuu** ya mtu aliyekomaa kweli: ana mwongozo wa maisha ndani mwake. Amazingatia pia kanuni za jamii na kusikiliza mashauri, lakini uamuzi wake unatoka ndani.

4. **Anajiongoza** kwa kuzingatia tunu alizojichagulia. Anaelekeza maisha yake upande fulani alivyoazimia. Katika kuamua la kufanya **anafuata tunu hizo, si mkondo** kama wanavyofanya kondoo.

5. **Anahusiana vema na watu** kwa sababu anawakubali, anawaheshimu na kuamini wanaweza kutenda mema. Anaelewa shida zao na kuwatimizia. Anawafanya wajisikie raha na kutokeza sifa zao. Mwenyewe anajisikia salama na kuwafanya washinde hofu zao na hivyo wakoma kwa urahisi zaidi.

6. **Anafanikisha mipango.** Ana mawazo ya kushangaza kwa kuwa mitazamo yake ni mipana na ya ndani zaidi. Mipango na miradi yake ni mingi, Lakini haogopi kujaribu wala kushindwa, kwa kuwa anatambua mambo yalivyo na yanavyoweza kurekebishwa. Hivyo mara nyingi anafaulu kufanya mambo yaye alivyoataka. Mambo yaliyo magumu kwa wengine, kwake ni rahisi.

7. **Anajiendeza aishi kwa ukamilifu.** Anatumia vizuri vipawa vyake vyote. Anafurahia mambo mbalimbali ya maisha na kufaidika nayo ili azidi kuijendezeza.

## PANDE MBALIMBALI ZA UKOMAVU WA MTU

### 1. Wa maono:

- anakubali maono yake bila ya kutawaliwa nayo;
- anaweza kuyajulisha ili kusaidiwa;
- anakabili magumu bila ya kuyaepa wala kuhangaiwa mno;
- si mtu wa kujikinga kila mara.

### 2. Wa nafsi:

- anasikiliza wengine, hatimaye anaamua mwenyewe bila ya wasiwasi mkubwa mno;
- anaweza kubadili uamuzi wake akipata habari mpya;
- anasema ukweli na kuchukua jukumu la uamuzi wake;
- anapokea uamuzi wa wengine.

### 3. Wa jamii:

- anaona wema wa wengine, asijifanye lengo la yote;
- anafungamana vema na wengine;
- ana marafiki wa kufaa;
- hawatgejemei mno ndugu zake;
- anafuata taratibu za jumuiya;
- analinganisha mahitaji yake na ya kikundi chake;
- yuko tayari kutimiza sheria halali hata zisipompendeza
- anafanya kazi hata ngumu kwa utulivu.

### 4. Wa maadili:

- anapokea mawazo mazuri na kuyaishi;
- anafuata malengo yake kwa sababu anayo ya kufaa;
- anatimiza busara, haki, nguvu na kiasi;
- yuko imara katika imani, tumaini na upendo.


### 5. Wa roho:

- anafungamana vema na Mungu na watakaturi;
- anamtegemea Mungu na kutimiza matakwa yake;
- anaelewa wito wake, anauthamini na kudumu kwa hiari kuuitikia.

## MAMBO YANAYOZUIA UKOMAVU

Binadamu anakusudiwa kukomaa, lakini hafanikiwi sikuzote. Tunawaona watu waliolemaa upande wa mwili, lakini wengi zaidi wamelemaa upande wa nafsi. Sababu ni kwamba mtu akikosa haja zake za msingi hawesi kustawi. Haja hizo zina nguvu sana, nazozisipotimizwa zinamuacha mtu kilema. Mchoro ufuatao unaonyesha mambo yanayompata hata akalemaa kinafsi:

1. Hatimiziwi haja za nafsi, ambazo ni za msingi kama zile za mwili, hivyo zisipotimizwa yanaanza matatizo.
2. Hajisikii vizuri, hata kama ni mtoto au haelewi, kwa kuwa mtu akihisi hapendwi, hatakiwi, hayuko salama, basi anajisikia vibaya mpaka ndani.
3. Anapatwa na wasiwasi unaofanya nafsi isistawi, hata kama mwili unaendelea kukua. Ndiyo sababu anashindwa kushirikiana vizuri na watu au anajitenga nao kwa kuona hawampi anayoyahitaji.
4. Kutokana na hofu hashiriki vizuri katika mambo yote. Anatambua kwamba akibaki peke yake hapati nafasi ya kupendwa, lakini anashindwa kukabili hofu yake.
5. Matokeo yake ni kwamba anajihisi hastahili kutimiziwa haja zake. Hatimaye anaweza akajichukia kama kwamba ndiye anayesababisha watu wasimtimizie haja zake.
6. Anafadhaika asijue la kufanya mbele ya matatizo hayo. Anashindwa kupata jibu kuhusu haja zake kutimizwa kesho: ikiwa leo hapati anayoyahitaji hata kwa watu wenye wajibu kwake, je, atayapata lini?
7. Anafuata njia za kujikinga na hofu hizo kusudi asiendelee kufadhaika. Moja ya njia hizo ni kusukuma ndani kabisa mwa nafsi yake yale yasiyompendeza yasielee tena katika kumbukumbu; lakini kadiri mambo hayo yalivyoshindiliwa ndani yanamvuruga na kujitoneza kwa matendo na maneno yasiyotarajiwa. Njia nyiningine ya kujikinga ni kutokubali hali halisi, yaani kukataa kukabili jambo la hatari au lisilopendeza. Njia nyiningine ni kuhamisha dhihirisho la ono fulani (hasira, chuki n.k.) limlenge mtu tofauti na yule anayekusudiwa. Njia nyiningine ni kuishi katika ndoto za mchana badala ya kuwazia hali halisi: mtu anajichorea akilini picha ya ulimwengu mwagine ambapo mambo yanakwenda anavyotaka, hata akaamini ndio wa kweli. Njia nyiningine tena ni kujitafutia visingizio ili kutosikia aibu moyoni: mtu anaweza akafikia hatua ya kumshtaki mwenzake kwa kosa alilolifanya mwenyewe. Njia ya mwisho ni kudai kwamba wengine ndiyo wenye hali aliyonayo mwenyewe asiikubali.
8. Kwa kuwa njia hizo hazimtimizii haja zake, hazimsaidii ila zinamtuliza kijuujuu tu kwa muda, yaani zinafunika matatizo yake badala ya kuyatatua. Mtu amejikinga isivyofaa, basi shida inabaki palepale. Hivyo mviringo usioelekea popote umekamilika kwa kurudia namba moja: mtu anahitaji bado kupendwa, kukubaliwa, kuthaminiwa na kuwa salama. Nani atamsaidia?



## DALILI ZA MTU ASIYEKOMAA

1. Anapurukusha tu na kulipua kazi mpaka asimamiwe.
2. Hatimizi vizuri wajibu wake kwa jumla, ni mtegezi.
3. Anachekachecha na kucheza wakati usiofaa.
4. Ana kiburi cha kitoto.
5. Hajui kujiheshimu wala kuwastahi wengine.
6. Ni mbishi, pia kwa makusudi, tena mlalamishi.
7. Hajui kulinda siri za nyumbani, ni mchongezi.
8. Hajali maonyo, anayachukua kimzaha.
9. Hakubali maoni ya wengine.
10. Si mnyofu wala hajui kujieleza wazi alivyo.
11. Anaogopa kutoa mawazo yake mbele ya watu.
12. Haamui kwa utashi imara.
13. Anafuata mkumbo.
14. Katika kuwapenda wenzake ana ubaguzi.
15. Anajipendekeza na kujipendea.
16. Anadai kubembelezwa na kufarijiwa.
17. Hana uvumilivu wala moyo mkuu.
18. Anatunza kinyongo.
19. Anakata tamaa kwa urahisi.

## SAFARI YA UHURU

Ndani mwetu mambo mbalimbali yameunganika na kufanya kazi pamoja tuwe tulivyo. Hasa **mwili na roho vimeunda kiumbe kimoja kizima**, yaani binadamu. Sehemu ya kwanza, inayoonekana, ni **mwili**. Mwili wetu ni wa ajabu, lakini **nafsi** ni ya ajabu zaidi: kwa **kumbukumbu** tunashika yaliyopita na kwa **ubunifu** tunaweza kujichorea picha za mambo tusiyowahi kuyaona, pia kubuni vitu vipya. Kwa **akili** tunaweza kujua na kuelewa mambo mengi; akili inakusanya habari mbalimbali, inazipanga na kuzipeleka kwa **utashi** ili uchague na kuamua. **Binadamu ni tofauti na wanyama** wote hasa kwa sababu **anaweza kuchagua** au kukataa kitu chochote chema au kibaya, **hata tunu** za maadili na dini na hatimaye Mungu.

Lakini **je, hiari yetu ni kamilii?** Tuache kwamba pengine watu wanatumia nguvu tusitende tunavyotaka. Tunachohitaji kuona ni kama ndani mwetu **mna mambo yanayopunguza uhuru**. Neno hilo linalelezwa na

kamusi kuwa "hali ya kutotawaliwa na mtu au nchi nyingine; hali ya kufanya mambo bila ya kuingiliwa". Je, maneno hayo yanaridhisha? Kadiri ya elimunafsia, **mtu huru hasa ni yule aliyekomaa**, kwa kuwa ametimia katika umbile lake asizuiwe na chochote. Mtazamo huo wa kibinadamu unakamilishwa na ule wa imani unaonyesha kuwa mtu huru hasa ndiye mtakatifu, yaani yule **anayeongozwa na ukweli na upendo katika yote**. Uhuru ni kazi. Maisha yetu yote ni safari ambayo tujifunze kuwa huru kweli kuanzia ndani. Hali hiyo haipatikani ghafla, wala kimuujiza, wala kwa kukua kiumri. Kutokana na udhaifu wa asili **tunakuwa huru polepole**, na kwa sharti la kufuata hatua zinazotakiwa. Kulingana na bidii tunazozifanya, mara tunaweza kufaulu, mara tunakuja kushindwa, kama vile mambo tunayokutana nayo mara ni ya kufurahisha na kutia moyo, mara ni ya kukatisha tamaa.

#### **Safari hiyo ina matatu** ya maana sana:

1. Uhuru kutoka vizuio.
2. Uhuru kwa ajili ya malengo.
3. Uhuru pamoja na wenzetu.

## **VIZUIO VYA UHURU**

Tuanze kuona vizuio vinavyotufanya tusiwe huru kabisa; lengo letu ni kutoka katika hali hiyo.

Vizuio vya kwanza ni maelekeo ya **silika tuliyorithi**. Sisi ni watoto wa watu: hatukuumbwa moja kwa moja, bali kupitia wazazi. Tumerithi maumbile yao, na kwa njia yao tumerithi yale ya akina babu na bibi na ya wazee wa kale kabisa. Tutake tusitake, tangu tutungwe tunaelekea kuwa sawa nao katika mema na mabaya, hasa sawa na mmojawao kitabia.

Vizuio vingine ni **mazingira** tunayoishi, yale tunayoyaona na tunayoyasikia kandokando yetu kuanzia utotoni. Huo pia ni **mkondo** unaotusukuma tutende namna fulani bila ya kupima na kuamua wenyewe kwa uhuru. Siku hizi mazingira yanategemea sana vyombo vya **upashanaji habari** ambavyo vinafanya ulimwengu mzima uwe kama kijiji kimoja tu, na utamaduni wake kuelekea kuwa mmoja.

Uhuru wetu unapunguzwa pia na **mazoea** yetu ya kufanya mambo kadhaa, tena kuyafanya namna ileile. Hivyo tunaweza tukashindwa kujiuliza kama ni mema au mabaya ili tuyaa che yakiwa mabaya.

Tena uhuru wetu unapunguzwa na **maono** (kuogopa, kukasirika, kufurahi n.k.). Hayo ni hali za nafsi zinazoonekana kwa nje kupitia mwili. Ni maitikio yetu kwa mambo au watu fulanifulani ambayo siyaamui yatokee. Kinyume chake yenyewe yanantisukuma kutenda au kutotenda namna fulani. Maono hayo yanaonyesha nathamini nini.

Mbali ya mambo yaliyo katika upeo wa ufahamu wetu, ndani mwetu **mna mambo tusiyoweza kuyafahamu** kwa kuwa yamefichika kabisa kama katika kisima kirefu. Baadhi yake ndiyo asili ya matatizo ya nafsi yetu. Tusipoyakibili kwa **ukweli** na kuyatoa **nje** hatutapona. Kweli kuna mengi kuliko macho yawezayo kuyaona.

#### **Mifano ya vizuio vya ndani:**

1. mambo ya ndani ambayo tunayatambua au la na ambayo yametokana na matatizo yasiyotatuliwa tuliyoyapata utotoni;
2. mazoea mabaya (majivuno, uroho, uasherati, uongo, ukaidi n.k.);
3. hali ya dhambi inayotutenga na Mungu;
4. kujisikia watu wasio na maana;
5. kujisikia wabaya sana, wenye makosa yote;
6. kuona haya kupita kiasi;
7. woga wa kujitokeza;
8. kuishi kijuujuu.

#### **Mifano ya vizuio vya nje:**

1. haja za mwili (chakula, kinywaji n.k.);
2. hali ya afya (vilema n.k.);
3. masharti ya mazingira na jamii (sheria, mila, desturi, miiko n.k.);
4. kutegemea wakubwa kama watoto wadogo.

## **KUWA HURU KUTOKA VIZUIO**

Ili tuweze **kuvishinda vizuio** hivyo inatubidi:

1. kuvitambua;
2. kujikubali tulivyo;
3. kutoridhika na uhuru tulionao tangu utotoni;
4. kutojidanganya kuwa tutaweza kupata uhuru kamili kwa urahisi.

**Tusiendelee kujitetea** kwamba, "si kosa langu, ni tabia yangu, siwezi kujishinda, sitabadilika, nashindwa kujirekebisha, huyu simpendi, bahati mbaya n.k.". **La sivyo tutabaki daima "watumwa** wetu wenyewe", na **matokeo yake** yatakuwa kama ifuatavyo:

- kujitafutia faida kwa ubinafsi.** Matokeo yake ni kutojitolea kwa upendo, kutojenga urafiki halisi, kutokuwa na lengo maalumu nje yangu, kusababisha matatizo mengi katika mafungamano na wengine, kutamani mno kufaulu, kutambulikana na kutawala n.k.
- kwategemea mno wengine.** Matokeo yake ni kujifanya mnyonge ili kuhurumiwa na kubembeleza, mara kujitafutia sifa, mara kuzikataa, kushindwa kuamua lolote n.k.
- kutafuta ukamilifu katika yote.** Matokeo yake ni kutokubali makosa, hitilafu na kasoro (hata za afya), kuogopa mno kukosa, kujitetea daima, kukandamiza wengine, kutaka kuonekana mtakatifu, kuogopa mno hukumu za watu, kutoridhika na mambo ya kawaida n.k.
- kushikamana mno na sheria.** Matokeo yake ni kujali sheria kuliko watu, kushikilia maoni hata kukataa ya wengine, kuwa mnafiki, mgumu, mkali, kutokuwa na huruma, kujisikia daima mdhambi asiyestahili huruma, kuhitaji kujitakasa kila wakati n.k.
- kuona mno haya.** Matokeo yake ni kutojiamini, kuogopa kuhukumiwa, kukosa raha katika kundi, kuwa mpweke, kujifungia ndani zaidi na zaidi, kukauka, kukata tamaa, kushindwa kujieleza, kukosa moyo wa kusema ukweli n.k.

Kama hatujatambua vizuio vya namna hiyo vinayotufanya watumwa, **tukumbuke** matukio yaliyopita, hisia zetu, mazoea yetu n.k. **Tujiulize:**

- mambo gani hasa yananizua nisiwe mwenyewe?
- Kulingana na mazingira yangu mambo gani yanaweza kunizua nisiwe huru kweli (nyumbani, kazini, mkutanoni n.k.)?
- Wanaonifahamu vizuri wananiaona kuwa huru au la? Kwa nini?
- Nimefanya jitihada gani niweze kuwa huru zaidi?
- Uhuru wa ndani nitaupata wapi? Lini nimewahi kujisikia ninao?
- Nafahamu watu wenyewe uhuru wa ndani kweli? Kwa nini nawaona hivyo?

## KUWA HURU KWA AJILI YA LENGO

Miguu yako inakufaa nini usipojua njia ya kwenda mahali? Vifaa vyako vina kazi gani usipofahamu nyumba ipi unataka kujenga? Utajiri wa upendo wako una faida gani ikiwa hujaamua utauelekeza kwa nani? Ina maana gani kujitawala kwa kuyashinda yasiyokufaa (maeleko au mazoea mabaya, vizuio n.k.) usipoelekeza uhuru wako kwenye wema fulani?

Basi, baada ya kujikomboa kutoka utumwa wa nje au wa ndani, ni kazi yako **kuulinda uhuru** uliojipatia, usije ukatalawiwa tena kwa njia tofauti. Uhuru wako **usikose lengo** lenye maana na ukweli, ukingojea mambo yatokee yanavyotaka bila ya wewe kujishughulisha. Kinyume chake, utambue ubora wa kutekeleza uhuru kama changamoto inayostahili uipokee, ubunifu wa mambo mapya utakaojitokeza katika utendaji wa bidii, uwezo wa kujiamulia kadiri ya lengo jema. Uhuru ni fursa kubwa ya kujijenga sawasawa, kufuatana na **tunu za maana**, kutekeleza **mpango kamambe kwa maisha** yako, kuitikia wito toka kwa Mungu, kutambua uhuru unavyoundwa na wajibu wa kutumikia watu, kujitawala kwa bidii na bila ya kurudi nyuma ili uwe **mwaminifu**, kujali utu wako na dhamiri yako na kuweza **kujitolea** kadiri ya tunu unazozithamini bila ya kudai kitu. Fanya uamuza wako wa msingi ambaa uwe daima na kipaumbele katika maisha yako na kuongoza maamuzi mengine mengi madogomadogo. Uhuru wako usiwe tena kuchagua kati ya mema na mabaya, bali **kuchagua mema yale yanayofaa zaidi** kwa utu wako na wa wenzako. Kisha kutambua tunu za maisha yako, polepole utatambua pia kuwa chemchemi na **msingi wake ni Mungu** mwenyewe. Bila yake uko bado katika hatari ya kutofikia uhuru wa kweli, au kutoudumisha au kutochuma matunda yake.

Uhuru wako utakamilika hasa kwa **kuwajibika kwa wengine**, kutokana na kuwathamini kama watu wanaostahili heshima na huduma yako. Hapo utakuwa macho kutambua wanayoyahitaji na utakuwa tayari kujitolea na ujuzi, mang'amuzi na vipawa ulivyo navyo bila ya kujali gharama (hata kama ni kutoa uhai wako) wala kurudi nyuma kwa lolote. **Kielelezo kikuu cha uhuru huo ni Yesu**, halafu mtume Paulo, aliyejichagulia tunu za maisha yake (Kristo na Habari Njema), halafu akajitoo mhanga kuzitekeleza. "Maana, ingawa nimekuwa huru kwa watu wote, nalijifanya mtumwa wa wote, ili nipate watu wengi zaidi... Kwa wanyonge nalikuwa mnyonge, ili niwapate wanyonge. Nimekuwa hali zote kwa watu wote, ili kwa njia zote nipate kuwaokoa watu. Nami nafanya mambo yote kwa ajili ya Injili ili kuishiriki pamoja na wengine" (1Kor 9:19,22-23).

## KUWA HURU PAMOJA NA WENZETU

Tukiongozwa bado na ubinafsi jitihada zetu hazitatosha kuondoa vizuio vyote vinayotufanya tusifikie uhuru wa mtu aliyekomaa. Tutapata uhuru huo ikiwa tu tunafungamana vizuri na jumuia. **Tutaupata pamoja na wale tunaoishi nao**, tukithaminiana na kuongozana katika safari ya kuelekea uhuru wa kweli. Tusipopiga hatua hiyo ya lazima tutazidi kustawisha ubinafsi wetu na kuwa mzigo kwa jumuia. Ili kupata maendeleo ya kweli ni lazima **tushirikiane** na kufanya bidii jumuia nzima katika kufuata lengo maalumu la maisha, kadiri ya alama za nyakati na mahitaji ya jamii. Kwa ajili hiyo tuwe tayari kuungana na wengine kwa kuachana na mazoea ya binafsi, uvivu na starehe, na kwa kupoakea mawazo yao katika kutekeleza mipango ya jumuia. Hivyo **polepole tutajisikia "sisi"**, tutaonja uzuri wa kuwa kitu kimoja na kushirikiana kikamilifu pamoja na **kuheshimu uhuru wa kila mmoja**.

## UPAMBANUZI WA SILIKA ZA NAFSI

Hapa hatuzungumzii tabia za kiadili bali **silika za nafsi**, yaani **jumla ya maelekeo ya ndani** yanayotokana na urithi, mazingira na utashi na ambayo yanaonyesha **namna maalumu ya kuwaza na kujitokeza**. Silika ni nydingi, kiasi kwamba toka zamani wataalamu **wamejaribu kuzipambanua wasikubaliane**. Baadhi yao wanasisitzia **mwili kama msingi wa silika** (k.mf. ya watu warefu wembamba, ya watu wafupi wanene, ya watu wenye umbo la wastani). Mtazamo huo una ukweli fulani, yaani **umoja wa binadamu** kama changamano la mwili na roho, lakini nafsi inaundwa zaidi na **matukio** ya maisha, hasa ya utoton: ndio yanayomuathiri mtu zaidi, pamoja na kwamba **anapaswa kurekebisha** daima silika yake. Kwa ajili hiyo ni muhimu ajifahamu ili **akuze sifa njema na kupunguza kasoro** zake. Katika kazi hiyo ategemee sana msaada wa Mungu: neema ina nguvu kuliko maelekeo yoyote ya umbile na inatenda maajabu, tunavyoona katika maisha ya **waliofikia utakatifu** kuanzia silika tofauti kabisa. **Neema haikomeshi umbile, bali inalikamilisha.**

Hapa tutadokeza aina mbalimbali za upambanuzi, kuanzia ya zamani zaidi, kwa kufuata tu **maelezo makuu** yanayokubaliwa na wengi. Kila aina inafaa zaidi kwa baadhi ya watu, yaani wale wanaolingana wazi na taswira yake mojawapo; kumbe ni vigumu zaidi kutambua na kupanga wale wenye silika za wastani. Hapo ni afadhali kukimbia aina nydinge ya upambanuzi. Kwa vyovytote **si rahisi** kupata mtu anayelingana na taswira fulani kwa **asilimia mia**: kwa kiasi fulani kila mmoja anaelekea taswira nydinge pia.

## AINA ZA SILIKA KADIRI YA WAGIRIKI

Labda asili ya upambanuzi huu ni mganga Hipokrate (aliyekufa mwaka 377 kabla ya Kristo). Zamani walidhani **silika nne** za msingi walizozainisha zinategemea kile kinachotawala mwili wa mtu, yaani nyongo, neva, damu au limfu. Dhana hiyo haikubalki tena, lakini wengiwengi wanaifuata bado upambanuzi huo kadiri ya jambo linalojitokeza zaidi katika silika ya mtu, yaani **hasira, huzuni, uchangamfu au upole**. Msingi wake ni jinsi yanavyochanganyikana kwa namna tofauti mambo mawili: **wepesi wa kuhemka na elekeo la kutenda**. Aliye na yote mawili kuliko kawaida ni mtu wa hasira. Aliye na lile la kwanza kuliko kawaida lakini la pili kidogo kuliko kawaida ni mtu wa huzuni. Aliye na lile la kwanza kidogo kuliko kawaida lakini la pile kuliko kawaida ni mtu wa uchangamfu. Hatimaye aliye na yote mawili kidogo kuliko kawaida ni mtu wa upole. Kwa kujibu maswali kadhaa tunaweza kujua **tunayo kwa asilimia ngapi**, na hivyo tunalingana na taswira mojawapo kwa kiasi gani. Jedwali linavyoonyesha, kila silika inapakanana nydinge mbili ambazo zinafanana nayo upande wa wepesi wa kuhemka au upande wa elekeo la kutenda, kumbe ni kinyume cha ya nne ambayo hailingani nayo wala upande wa wepesi wa kuhemka wala upande wa elekeo la kutenda.

HASIRA	HUZUNI
UCHANGAMFU	UPOLE

### A. SILIKA YA HASIRA

Mwenye tabia hiyo anaitikia mambo kwa **kusisimka mara kwa nguvu**, halafu athari yake **inadumu** muda mrefu nafsi mwake.

**Sifa njema ya silika hiyo tajiri** sana ni akili kali, uwezo wa kukusanya mawazo, utashi imara, udumifu, **utendaji mwingi**, moyo mkuu, ufadhili. Anachukia pumziko na upotevu wa muda. **Ana nia na mambo**; kila mara anavutiwa na **mipango mikubwa** na kuanza **mara** kuishughulikia, **asirudi nyuma** mbele ya matatizo. Mara nydingi anakuwa **kiongozi**, mtawala, mtume mkubwa.

**Kasoro zake**: msimamo wake unamuelekeza kuwa **mgumu**, kutojali, kutakabari, kuwa kaidi, kukasirika. Mara nydingi ana **uchu wa madaraka** na ukuu. Katika mafungamano hana ulaini wala **haelewi sana uchungu** wa wengine. Msisimko wake katika utendaji na hamu kubwa ya kufanikisha mipango yake vinamfanya **akanyage vipingamizi** vyovytote na kuonekana hana moyo. Akipingwa anaweza akawa **katili**; akishindwa anaweza akatunza **chuki** hadi saa ya kulipa kisasi. Miguso yake inazama katika **ukali wa hisia** zake.

**Asitende harakaharaka**, asiamini misukumo ya kwanza kutoka moyoni. Atekeleze **unyenyekevu halisi**, ahurumie walio dhaifu, asimdhaliilishe yejote, asitawale kwa mabavu. Akifaulu **kutawala milipuko** ya hasira yake na kuelekeza vizuri nguvu zake anajipatia upole bora na kuwa **wa thamani sana**. Kazi ngumu zinafanikiwa mikononi mwake kutokana na utashi na udumifu alionao. Kwa urahisi fulani anaweza akafikia **utakatifu mkuu**. Walikuwa na silika hiyo mtume Paulo, Mt. Jeromu, Mt. Ignasi wa Loyola, Mt. Fransisko wa Sales na wengine wengi.

### B. SILIKA YA HUZUNI

Mwenye tabia hiyo anaitikia mambo kwa **msisimko amba mwanzioni ni dhaifu** na wa shida, lakini unakuwa wa nguvu na wa dhati akiendelea kuathiriwa; tena kwa kawaida ni wa muda mrefu: **hasahau kwa urahisi**.

**Sifa njema: miguso** yake ni **ya ndani, lakini haijitokezi** sawasawa. Kwa kawaida ana akili kali na ya kina, akiivisha mawazo kwa **kutafakari kwa utulivu**. Anaelekea kukaa **pweke** na kufuata ibada na maisha ya kiroho. Hivyo anaweza akawa **msomi mkavu** anayejifungia kutafuta elimu au **mwanasala** anayezama katika

mambo ya Mungu. Anavutiwa na sanaa na kufaa upande wa sayansi. Akipenda **si rahisi kukata upendo**. Ni mwepesi **kuhurumia na kufadhilli** (hasa wagonjwa), akijitolea hadi ushujaa. Anapatwa na uchungu akiona watu baridi na wasio na shukrani. Utashi wake unategemea hali ya mwili: ni dhaifu sana akiishiwa nguvu, kumbe una juhudhi akiwa na afya na kupata furaha kidogo. Ni mtu wa kiasi, **havurugwi na maono**.

**Kasoro:** hasa ni elekeo kubwa mno kwa huzuni. Anaelekeea kutarajia daima mabaya, **kuona magumu tu**, kuzidisha ukubwa wa matatizo. Kwa hiyo anakwepa watu, hajitokezi, **ana aibu**, hajiamini, ana wasiwasiju ya maadili yake, **anashindwa kuamua**, anakata tamaa. Anasitasita kwa **kuogopa atashindwa**, hivyo anapoteza nafasi nzuri nydingi. Anateseka na bila ya kukusudia **anasababisha wengine pia wateseke**. Anaweza akapatwa na donda bayaa nafsini mwake, anapoonja peke yake uchungu wote, kwa kukosa ari ya kuutokeza. Hali hiyo ikizidi na kumfanya adaidai mambo ya pekee au kutokeza uchovu wa neva, hafai kwa utawa.

Mwenye silika hiyo anapenda **kujieleza vizuri** katika uongozi wa kiroho, lakini hawezikwa sababu ya kujikusanya mno kwa ndani. Kiongozi amuelewewi hivyo na kutumia busara na adabu sana. Amsaidie **kumtegemea Mungu**, kukabili maisha kwa amani na **kutarajia mema**. Pia aamini zaidi kuwa anafaa kwa makuu. Kwa kutumia elekeo lake kwa fikara aelewewi hana sababu ya kuguswa mno, kuogopa na kujitenga. Pengine apumzike na kula vizuri. Hasa aachane na wasiwasiju na woga kwa kuweka maazimio imara na **kulenga makuu** kwa moyo na tumaini. Walikuwa na silika hiyo mtume Yohane, Mt. Bernardo, Mt. Alois Gonzaga, Mt. Teresa wa Mtoto Yesu na wengineo.

### C. SILIKA YA UCHANGAMFU

Mwenye tabia hiyo **anasisimka kwa urahisi na nguvu** mbele ya chochote, lakini itikio hilo ni la **muda mfupi**. Kumbukumbu ya mambo yaliyopita haisababishi msisimko mpya. Silika hiyo ni **kinyume cha ile ya huzuni**: haina wepesi wa kuhemka, bali inaelekeea utendaji.

**Sifa njema:** ni msemaji, **mfurahivu**, **mwenye heshima** kwa wote, msikivu na mtiifu kwa wakubwa, **mnyofu na wazi** (pengine kupita kiasi). Anaelekeea kusifu mno kuliko kulaumu. Anashangaa kuona watu wakichukia utani wake usiofaa, kwa kuwa anaudhani mzuri kabisa. **Hajui ukaidi**. Anaguswa na kutiwa **huruma na matatizo** ya watu, halafu **anajitolea** kweli. Wema wake unapendeza, ari yake inaambukiza na **kuvutia wengi**. Kwa kuwa anafurika mapendo, ni mwepesi kufanya **urafiki** na kuufuata kwa bidii. Akichukizwa anaitikia pengine kwa ukali na matusi, lakini anasahau yote mara, **hatunzi kinyongo**. Anajua kushughulika kwa kuwa **anakabili maisha kwa utulivu**, akitarajia daima mazuri, asirudi nyuma mbele ya matatizo. Ana kumbukumbu na **ubunifu mkubwa**, hivyo anafaulu katika sanaa na mahubiri, lakini hawi mwenye hekima zaidi, kwa kuwa **akili yake ni nyepesi**, inadaka kwa urahisi, ila **haina kina**.

**Kasoro zake ni kubwa** kama sifa njema: hasa ni ujujuu, ugeugeu na tamaa za mwili. **Ujujuu** unatokana na uerevu na urahisi wa fikra unaomfanya adhani ameelewa mara suala lolote, kumbe amelihishishi tu. Ndiyo sababu tathmini zake ni za harakaharaka, mara nydingi si sahihi, pengine hazina ukweli wowote. **Katika masomo ni mvivu:** anapenda upana wa ujuzi, anaoweza kuuonyesha ili kujipatia sifa, kuliko kina chake. **Ugeugeu** unatokana na ufupi wa muda wa maitikio yake: mara anacheka, mara analia; ghafla anaacha uchangamfu mkubwa na kupatwa na huzuni kubwa vilevile. **Anatubu makosa** mapema na kwa moyo, lakini **anayarudia** katika nafasi ya kwanza, kwa kuwa anasisimka mno, hana nguvu na moyo ashinde **tamaa za mwili** zinazostawi kutokana na **umotomoto** wa silika hiyo. Kwake ni vigumu kutawala macho, masikio na ulimi wake. Katika sala anatawanya mawazo kwa urahisi. **Hapendi sadaka**, kujikana, kujitahidi kwa kudumu. Vipindi vya bidii kubwa vinafuatwa na vingine vya kuvunjika moyo.

Aelekeze umotomoto wa **mapendo yake kwenye lengo bora**: akichanganyikiwa na Mungu atakuwa mtakatifu mkubwa, kama mtume Petro, Mt. Augustino, Mt. Teresa wa Yesu, Mt. Fransisko Saveri na wengineo. Lakini ni lazima **ashinde kabisa kasoro** zake. Dhidi ya ujujuu **azoe kutafakari** na kupima mambo yote, aelewewi masuala pande zote, kwa kutabiri matatizo yanayoweza kutokeza, **asitarajie mema tu**. Dhidi ya ugeugeu asitegemee maazimio tu, hata akiyaweka kwa moyo, kwa kuwa atayavunja mara. Amtii kabisa kiongozi wa kiroho, **ashike ratiba** ambayo iwe imekubaliwa naye na kupanga yote **bila ya kuacha nafasi kwa utashi wake dhaifu**. Ajitafiti kwa bidii na **kujiadhibus vikali** kwa makosa. Katika sala asitafute faraja za kihisi, bali **adumu katika ukavu** pia. Dhidi ya tamaa mbaya **awe mwangalifu daima**, akikwepa nafasi yoyote ya hatari, akikusanya mawazo na kutawala hisi za ndani na za nje, akizuia hasa macho kwa kukumbuka mang'amuza ya kusikitisha. Amuombe Mungu kwa unyenyekevu na udumifu neema ya usafi ambayo inatoka mbinguni tu.

### D. SILIKA YA UPOLE

Mwenye tabia hiyo **anasisimka kidogo** tu. Itikio lake kwa lolote ni dhaifu au halipo kabisa. Haatiriki nafsi ni mwake kwa kuwa **alama yoyote inafutika** mara.

**Sifa njema:** anatenda **polepole lakini kwa mfululizo**, mradi asidaiwe juhudhi kubwa mno. Hatawaliwi na maono. **Hachukizwi** sana na matusi, maradhi wala kutofanikiwa. Anadumu kuwa **mtulivu**, **mwenye kiasi na busara**. Anajua kukabili maisha, kwa sababu **anafikiri sana na kutenda kwa hakika**, akifikia malengo yake pasipo kutumia nguvu zaidi, kwa kuwa **anaondoa vipingamizi** badala ya kuvivunja. Anazungumza kwa haki na namna ambayo **inaeleweka na kuvutia**. Ana moyo mwema, ingawa unaonekana baridi. Ikiwa lazima atajitolea hata kishujaa, lakini si kwa ari na kwa kusukumwa na **umbile lake la uvivu**. Hajitokezi. Kimwili ana **sura ya kupendeza**, tipwatipwa, mwendo wa taratibu. Pengine akili yake ni kubwa sana. Anafaa kwa utafiti wa sayansi

unaodai **subira** ya muda mrefu, si kwa ubunifu wa mambo mapya. Mt. Thoma wa Akwino kwa kufaidika na sifa bora za silika hiyo alifanya kazi kubwa kwa utulivu na utaratibu.

**Kasoro:** anapoteza nafasi njema nyingi kwa **kuchelewa** kuzitumia. Hata katika shida za haraka ni kama amesinzia. Hajali sana yanayotokea nje yake. Anaishi kama kwa **ubinafsi. Hafai kuagiza** wala kutawala. **Hapendi matendo ya toba** na malipizi: hakuna hatari kuwa atajidhuru kwa hayo!

Anahitaji kuwa na msimamo (wa imani) na kujilazimisha **afanye juhudzi za mpango** na za kudumu. Polepole atafika mbali, mradi **aache kusinziasinzia** na kupiga uvivu. Badala yake alenge makuu. Ajirekebishe si kwa kujizua (inavyompasa mwenye silika ya hasira iliyo kinyume chake), bali kwa kujichochea na kuamsha nguvu zilizosinzia.

## AINA ZA SILIKA KADIRI YA SUFII

Upambanuzi huu pia ni **wa zamani**, ila mwishoni mwa karne XX imechunguzwa na **kutengenezwa upya** na wanasaikolojia waliouita **enneagram**, yaani **mchoro wa silika tisa**, ambazo zinaitwa kwa **tarakimu** fulani na kupangwa katika duara. Hizo **zinahusiana** kwa namna mbalimbali, lakini hasa ni kwamba tatu (5, 6, 7) zinifuata zaidi mawazo ya **kichwa**, tatu (2, 3, 4) hisi za **moyo**, na tatu (8, 9, 1) misukumo ya **matumbo**. Kila mtu anaweza kutumia vitovu vyote vitatu, lakini polepole tumependelea kimojawapo hata kikatawala vingine. Hivyo kwa kutegemea urithi na mazingira tumepoteza uwiano.

Hakuna namba nzuri au mbaya zaidi: kila moja ina utajiri na udhaifu wake. Tusichague namba fulani kwa sababu tunaipenda, bali tujaribu kujua na kupoeka ukweli juu yetu. Ni rahisi kujitambua kwanza tupo katika kundi lipi kwa kuchunguza tunavyojisikia tukifikiria tunatakiwa kuishi katika **miji mitatu** ifuatayo, ambayo ni ya kubuniwa, lakini tuichukue kama ni ya kweli.

### A. MJI WA KICHWA

Umejengwa kwa **mpango kabambe**: majengo yote yanalenga **kufaa tu, hayana pambo** lolote lile, tena karibu yote yako **sawa**. Vioo vyake ni vyeusi ili watu wa ndani **waveze kuona kila kitu** nje **wasionekane** wenye. Katika mji huo utajisikia daima unachunguzwa na wenyeji. Kwa namna fulani **hofu** ndiyo ono linalotawala, hivyo wanahitaji **kujikinga** na watu na hatari. Nyumba nyingi zimezungukwa na kuta ndefu zenye mageti mazito, watu wasije wakaingia bila ya **ruhusa maalumu**.

Barabara zote zinakwenda **wima** tu na kupangwa **kama jedwali**. Kuna vibao vya kuelekezea, navyo vyote vimechongwa kwa **usanifu** na kuandikwa namna **inayosomeka** kwa urahisi. Barabara zina taa za kutosha kuangazia wanaotembea usiku. Lakini hakuna watu wengi njiani, na wale wachache **wanakwenda zao** bila ya kusimama kwa maongezi mrefu: kila mmoja anaonekana **kufuata mawazo yake muhimu asitake kusumbuliwa**.

Pamoja na hayo **wanajali sheria** za usalama barabarani na **adabu njema**, wakiwaachia wenzao njia pasipo ukorofi. Pamoja na kuwa na nidhamu ya hali ya juu, wanaweza kupoeka na kusaidia wenzao kwa **ukarimu**, lakini bila ya kushirikisha maoni yao **wala kutokeza hisi** zao. Usafi ni mkubwa, kwa kuwa watu wa kichwa wanapenda **kila kitu kisiwe na doa**.

Kuna **shule nyingi** ajabu, za kila aina, hata vyuo vikuu; tena wanafunzi wake si watoto na vijana tu, bali watu wa makamo na **wazee pia**. Vilevile **maktaba ni nyingi**, na watu wanaingia na kutoka mfululizo huko wakibeba **vitabu**.

**Mtume Thoma** ndiye msimamizi wa kanisa kuu: kama yeye, Wakristo wa huko wanaonekana kudhani imani ni kuona. Ndani ya kanisa, benchi zimepangwa mistarini kwa **utaratibu kamili**, nazo zimejaa vitabu vya ibada na tafakuri.

Pamoja na hayo, **watu wa kichwa wanatofautiana pia**. Katika mji huo tuliwakuta:

- **Bibi sita, mshikasheria**, ambaye alitupokea vizuri nyumbani na kuzungumzia watoto wake anaowapenda sana. Ameshawapangia maisha ya mbeleni akisukumwa na hofu ya kuwa wataweza wakapatwa na matatizo yasiyoshindikana. Hasa alionyesha kuogopa wakubwa wake wote, hata yuko tayari kuwatii daima na kuwakubalia bila ya kuchanga neno lolote. Anafanya kazi vizuri kwa kutii mamlaka, si kwa kupenda. Mwenye nyingi anashindwa kuchagua, kuamua na kujituma. Anachotaka hasa ni **kuwa mwaminifu**.

**Kilema chake:** Woga. **Matatizo yake:** kujivunia utiifu wake, kuogopa mabadiliko, kuwa mgumu, shupavu na jeuri, kuhukumu haraka, kutovumilia. **Utatuvi:** kutambua kazi ya Roho Mtakatifu, kuwa tayari kwa mambo mapya, kukubali mabadiliko yanawezekana, kuzingatia roho ya sheria, kupoeka mapungufu ya wengine, kujitosa zaidi hata katika mambo yasiyo wazi. Asifuate mwelekeo wa kufanana na namba 3, bali aende kinyume na kujitahidi kufanana na namba 9.

- **Bwana tano, mchunguzi**, ni mtu wa nadharia. Anapenda kukaa kimya, kutazama yote, kuwasoma wengine, kujipatia ujuzi mkubwa zaidi na zaidi, kusoma na kusikiliza kwa makini anaowaona wanamzidi elimu. Lakini mwenye nyingi anahitaji msukumo mkubwa mpaka akubali kutenda, kutoa, kushirikisha ujuzi wake. Baadaye anashangaza kwa jinsi anavyoweza kueleza mambo kinaganaga kwa mpangilio mzuri. Hasa hapendi mikutano ya burudani. Anachotaka hasa ni **kuwa na hekima**.

**Kilema chake:** Choyo. **Matatizo yake:** kulaumu, kuchoma moyo hata kama ni kwa utani, kutojali wengine, kuwa mchoyo, kujitafutia raha. **Utatuvi:** kushirikisha zaidi nafsi, vipawa na muda wake, kujumuika na wengine,

kuonyesha na kueleza hisia za moyo wake, kukubali uwezo wake, kubuni na kuanzisha mambo. Asifuate mwelekeo wa kufanana na namba 7, bali aende kinyume na kujitahidi kufanana na namba 8.

• Kumbe sherehe fulani ndiyo nafasi tuliyokutana na **bibi saba, mfurahivu**. Huyo hawesi kuvumilia mwininge anune, hivyo yuko tayari daima kuigiza na kuchangamsha watu. Vilevile hapendi mazungumzo mazito juu ya hatari, shida na matatizo, hivyo akiyasikia anayakatisha mara na kuanzisha mengine ya burudani. Anapenda kufanya mipango mingi, pasipo hakika ya kuitekeleza kweli; akishindwa atadai wengine waitimize badala yake. Anavaa nguzo zinazomtia uzuri. Anachotaka hasa ni **kupendeza**.

**Kilema chake:** Ulafi. **Matatizo yake:** kuwa mlafi, kutokubali maumivu, kuepuka majukumu, kutofutilia mambo madogomadogo, kufungamana kijuujuu tu, kukosa subira, kuahirisha "mpaka kesho". **Utatuvi:** kuishi katika ukweli wa maisha, kuangalia matukio ya sasa, kukabili magumu kwa ustahimilivu, kutimiza kazi na mpango mpaka mwisho, kukubali mipango ya wengine na kujihusisha nayo. Asifuate mwelekeo wa kufanana na namba 1, bali aende kinyume na kujitahidi kufanana na namba 5.

## B. MJI WA MOYO

Umejengwa **bila ya mpango** wowote: kila mtu amejijengea popote alipoona nafasi ni nzuri kwa **kuhusiana na watu**. Hivyo nyumba zimesimama **karibukaribu, bila ya mipaka** wala mageti, zimezingirwa na **maua mengi** ambayo katikati yake kuna matangazo yaliyoandikwa kwa **usanii**. Mengi yake ni ya sherehe, ngoma na **burudani** mbalimbali.

Barabara zinazoziunganisha nyumba hizo **zinatumika sana**, tena sana. Watu wanaonekana wazi kupenda mafungamano, urafiki, **maisha ya kijamii**. Wanajali sana **sura** yao, kwa hiyo wanapenda **kuvalia mitindo mipyä** na ya pekee, kuzungumzia uzuri, urembo n.k. Pamoja na hayo wengi wamevaa **sare** ya unesi na ya **huduma** nyingine. Kuna makao mengi ya **vyama na kujitolea**, mbali ya sinema nyingi.

Kanisa kuu msimamizi wake ni **Mt. Marta**, nalo ni la pekee: kuta zake **zimepambwa sana** nje na ndani, na badala ya benchi kuna **mito**, makochi n.k. Ibada zinaonekana nzuri na za dhati, kwa kuwa waamini wanasali wanavyojisikia **kutoka moyoni** kuliko kwa kufuata vitabu na taratibu rasmi.

Pamoja na hayo, **watu wa moyo pia wanatofautiana**. Katika mji huo tuliwakuta:

• **Bibi mbili, mtoahuduma**, aliyetualika kwa chai na kutuonyesha anavyojali raha ya watu hata hakuweza kukaa nasi walau kidogo. Pamoja na kutuhudumia alipaswa kuitikia simu mfululizo, kwa sababu wengi wanamtafuta awasadie. Mwenyewe anafurahia sana jambo hilo, ila mara kadhaa analalamika akisema, "Mbona nadaiwa kila kitu mimi?". Anazidisha hisia zake kwa wengine, akiwaonyesha anavyowapenda, akiwabembeleza hata kuwatawala na kuwatumbia kwa faida yake. Upande wake anadai sana sifa na shukrani; akizikosa anadhani kuna uhasama dhidi yake. Tulipofaulu kuongea naye alipata habari nyingi kutoka kwetu, lakini hakujifahamisha kweli. Basi, tuligundua anavyotaka kujitawala asiweze kukubali yeche naye naye anahitaji msaada, wala kuuomba. Kwake ni vigumu kujifahamu kwa dhati. Anachotaka hasa ni **kusaidia wote katika yote**.

**Matatizo yake:** kujivuna, kuwa mjanja na mdanganyifu, kukosa subira, kujiona mkombozi, kumiliki wengine. **Utatuvi:** kukubali mahitaji yake, kupokea msaada, kuacha wengine wawajibike, kutambua mahitaji halisi, kutodhani bure kwamba ametupwa. Asifuate mwelekeo wa kufanana na namba 8, bali aende kinyume na kujitahidi kufanana na namba 4.

• **Bibi tatu, mtatutavyeo**, mkuu wa ofisi fulani. Tilitaka kumuona atueleze kuhusu shoti iliyotokea. Basi, karani wake hodari alituizingiza kwake bila ya kucheleva. Mara akaanza kuzungumzia hali ya ofisi akisisitiza bila ya kuchoka kwamba shoti yoyote haikuweza kutokana na kosa lake, bali mwenyewe amesharekebisha mengi, na kwa hakika baada ya muda mfupi yote yatakwenda sawa. Ni mtu wa juhudi sana, mshindani asiyekubali kushindwa. Ana uwezo mkubwa wa kujumuisha watu katika kazi ya pamoja. Anaonekana kujiamini, lakini hapendi kuonyesha miguso yake, wala udhaifu wowote. Anashughulikia sana afya yake lakini anashindwa kutambua hisia zake na anazitupa juu ya wengine. Anaweza akadanganya mradi afaulu, kwa sababu anachotaka hasa ni **kufanikiwa**.

**Kilema chake:** Udanganyifu. **Matatizo yake:** kupenda ubatili, kuwa mjanja, kufuata njia yoyote ili kufikia lengo, kutokubali kushindwa, kutoamini wengine. **Utatuvi:** kujikubali alivyo badala ya kuangalia kazi tu, kujitahidi kuwa namna fulani kuliko kuonekana na kutenda, kugawa madaraka, kukubali mengine hayawezekani, kukiri ameshindwa. Asifuate mwelekeo wa kufanana na namba 9, bali aende kinyume na kujitahidi kufanana na namba 6.

• **Bwana nne, msanii**. Ingawa ni mtu wa makamo hajaoa. Uhusiano wake na wengine ni mgumu, unapitia sanaa, alama na mifano. Nyumba yake ni nzuri sana, ina picha nyingi ukutani. Alipika mwenyewe na kupanga chakula namna ya kupendeza. Mezani tulifurahishwa na miziki myepesi. Anaeleza wazi na kwa dhati kwamba, "hakuna anayeonja miguso mbalimbali kama mimi". Anapenda mazuri na kuweza na kutaka amshirikishe yejote. Ila mazungumzo yake yalielekea kulilia mambo yaliyopita, hata huzuni ikatujia. Anajidanganya kuhusu ukweli wake. Anachotaka hasa ni **kuwa wa pekee**.

**Kilema chake:** Kijicho. **Matatizo yake:** kujiona mwema kuliko wengine, kuwashusha, kujitafutia makuu, kujisifu, kuwa na vivu, kukata tamaa, kunung'unika mno. **Utatuvi:** kutambua vipawa vyta wengine, kufurahia sifa wanazopewa, kusikiliza kuliko kusema, kumtia moyo anayeshindwa kusema, kufurahia mambo ya kawaida ya kila siku. Asifuate mwelekeo wa kufanana na namba 2, bali aende kinyume na kujitahidi kufanana na namba 1.

## C. MJI WA MATUMBO

Watu wake **wanapendelea historia na utamaduni wao**: ndio sababu kati ya majengo ya kisasa, ambayo ni sahili na ya kufaa kwa starehe, yapo mengine ya zamani yanayoonyesha uzuri wa wakati uliopita, na vilevile nyumba kadhaa za makumbusho. Sehemu kubwa ya ardhi hailimwi, ila kando ya nyumba kuna **mabustani** ya mboga badala ya maua.

Watu wa mji huu wanavaa nguo yoyote **wasijali urembo**. Hata chakula kinachaguliwa kulingana na **manufaa kwa afya** kuliko ladha. Ni **watu wa kelele**, wanapenda kusema kwa sauti kubwa, kusalimiana motomoto, kupiga muziki na ngoma. **Hawajali hukumu ya watu** kuhusu namna yao ya kusema, kuvaau au kupanga nyumba.

Wanatia maanani **haki** za binadamu, mahitaji ya kila mtu na hifadhi ya mazingira, kiasi cha kuona uchungu sana mambo hayo yakikosekana. Hata barabarani ni rahisi kukutana na kundi la watu wanaoshirikisha maoni yao juu ya mambo ya haki. Wanafuata na kuheshimu **mashindano**. Hasa wana busara ya kidunia.

Msimamizi wa kanisa kuu ni **mtume Paulo**. Mlangoni pa kanisa kuna orodha ya **mahitaji ya watu** ili kila mwamini atoe msaada anavyosukumwa kwa ndani.

Mjini huku pia tulikuta watu **tofauti**:

- **Bwana nane, mtawala**, anayependa kuongoza. Anajua uwezo wake wa kusababisha mambo mbalimbali hata maishani mwa watu wengine. Anawasukuma wanaomzunguka wajitolee kufanya kazi za hiari, hata mara nyingi ni kama anawalazimisha. Haogopi kumkabili yeyote, anatenda kwa nguvu, pengine kwa ukorofi. Hawezi kuishi bila ya kupigania haki yake na ya ulimwengu mzima. Hawezi kupokea chochote anachokiona si halali. Anaogopa kukubali hisani au miguso yoyote ndani mwake, akitisikia anaweza kuishi vizuri pasipo "upuuzi wa namna hii" (anavyosema). Anachotaka hasa ni **kuwa na nguvu**.

**Kilema chake:** Uzinifu. **Matatizo yake:** kuwa na kiburi, kukasirika vikali, kuchoma moyo, kutawala kwa maneno, kutupa wasioweza. **Utatuvi:** kukubali mambo yalivyo, kutambua hisia zake, kujipokea na kupokea wengine, kuvumilia wengine wasiokubaliana naye, kutohukumu, kuwa mpole kwake na kwa wengine, kuwawezesha wafanye, kustawisha wema alionao. Asifuate mwelekeo wa kufanana na namba 5, bali aende kinyume na kujitahidi kufanana na namba 2.

- **Bibi tisa, mpendaamani**, anayesikitika mno kusikia maneno makali, hivyo anajitahidi mara kuwatuliza aliye yatoa na aliyambiwa. Anajaribu kueleza kwamba sababu ya mlipuko wa hasira si wenye. Katika kuleta amani ana kipaji cha pekee. Hapendi ghasia wala haraka; anachelewa karibu kila wakati. Hana bidii, kwa sababu anaridhika na maisha yalivyo, kama kwamba hana lengo maalumu. Ila anajitafutia amani na raha hata kujipatia vingi kwa gharama asije akahitaji tena kwenda kununua. Anachotaka hasa ni **kutulia**.

**Kilema chake:** Uvivu. **Matatizo yake:** kustahimili mno, kukosa shauku, kutojihusisha, kusikia watu bila ya kuwasikiliza, kuahirisha kazi. **Utatuvi:** kujikaza, kujihusisha, kuamua, kutambua na kuonyesha hisia, kujithamini na kujali wengine. Asifuate mwelekeo wa kufanana na namba 6, bali aende kinyume na kujitahidi kufanana na namba 3.

- **Bwana moja, mdaiukamilifu**, ambaye kazi yake maalumu ni kusahihisha, kukosoa na kufichua uovu wake na wa ye yeyote yule. Kwake haki inawafanya wote wawe sawa, asikubali kupendelea wakubwa kwa sababu tu ni wakubwa. Anaona ulimwengu kama mkusanyo wa kasoro, ambazo ni kazi yake mwenye kuzirekebisha hata katika mambo madogomadogo. Anapenda kukosoa lakini pia kukosolewa kwa haki. Ni hakimu mkali asiyekubali kusubiri muda unaohitajika kukua. Kabla hajaanza kufanya kitu, anahitaji kuwa na hakika ya kukifanya vizuri. Anadai ukamilifu daima tena mara. Kwake ni shida kubwa kujipokea alivyo pamoja na kasoro zake. Hata akisema bila ya kelele, sauti yake inatokeza hasira iliyomo kwa wingi ndani mwake. Kwa kuwa anaona aibu sana kuonyesha, anaihifadhi ndani hata inakuwa kinyongo. Anachotaka hasa ni **jithada bora za kurekebisha yote**.

**Kilema chake:** Hasira. **Matatizo yake:** kujivunia ukamilifu, kukosa subira, kuwa shupavu, kuhukumu, kutosikia ya wengine, kutopenda kushirikiana nao katika majukumu. **Utatuvi:** kukubali mipaka yake, kutambua na kukubali hasira yake, kupokea wengine walivyo, kutumaini mambo yatakwenda vizuri, kufurahia hatua ndogondogo. Asifuate mwelekeo wa kufanana na namba 4, bali aende kinyume na kujitahidi kufanana na namba 7.

## AINA ZA SILIKA KADIRI YA C. G. JUNG

Kati ya michango mikubwa aliyoitao mtaalumu huyo wa Uswisi (1875-1961), mmojawapo ni kuainisha **makundi mawili** ya watu kadiri **wanavyo elekeza nguvu za nafsi** yao ndani mwao (wandani) au nje yao (wasondani).

- **Mndani** anathamini **ubora wa utendaji** kuliko wingi wa vitendo. Anahitaji **faragha** ambapo atafakari mambo, ajue sababu zake na kuyapanga kichwani. **Utafiti** na msukumo wa ndani ni vya lazima kwake. Anawaza sana kabla hajatenda, kiasi kwamba **pengine hatendi**. Mbele ya matatizo anasema, "Hakuna haraka kuyatatua". Mbele ya mahitaji ya watu **anasitasita** mpaka ajue ni ya kweli. Anapendelea kufuata dhamiri yake, kujitegemea katika shughuli, kusali na **kufanya mambo peke yake**. Kukutana na wengi kunamchanganya, na mbele ya wageni anaonekana mnyonge. **Anajisetiri** na kuficha hali yake isipokuwa kwa marafiki wa dhati.

Kwake ni vigumu kushirikisha. Ni **msikilizaji** kuliko msemaji. Akisema kwa kawaida hazungumzii **yale yanayomhusu**. Akisimulia anapenda kuwa mwangalifu. **Hakinai shughuli ileile** hata akiifanya muda mrefu. Anapaswa kuangalia asijitafutie raha yake ya ndani, bila ya kujali wengine.

• **Msondani** anavutwa zaidi kutenda na kujitolea kwa wengine. Tangu utotonu anaonyesha kuwa anahitaji **utendaji**, kuona matukio mengi na hata kuwa na **kelele** za kutosha. Daima anapenda kuwa **kati ya watu na mambo**. Anajihuisha mara na matukio mapya na kuitikia mahitaji ya watu. Anapenda kuona matokeo mazuri ya kazi zake, hatimaye anaweza akajivunia. Si mvumilivu kufanya kazi ndefu. Anazifanya **haraka**, pengine bila ya kufikiri. Anapenda **mabadiliko** na kuchoka upesi akibaki peke yake. Anasaidiwa na vitendo vya liturujia, sala ya kijumuia, kushirikisha mawazo juu ya Injili, kutoa maombi ya hiari. Kumbe ni vigumu kwake kujitafutia nafasi za sala ya moyo. Anapenda malimwengu na yanayoambatana na wengine, "unaonaje, unasemaje, unafanyeje?". Anajionyesha ni nani ulimwenguni, ni **mwelesi kusema** na kutambua mambo. Anapenda **kujilikana**, kuwa na marafiki wengi. Ni **mcheshi**, anasalimia upesi, anapenda kuchanganyikana na watu. Anajitambulisha kwa wageni kabla hao hawajitambulisha. Yuko **tayari kueleza maisha yake** mara anapokutana na watu. Anapenda kujua wengine wanamuonaje. Anapenda kueleza kwa sauti kuliko kwa maandishi. Ni mvivu kujibu barua, lakini mwepesi kujibu simu.

Watu wa **makundi hayo yote mawili** katika utendaji wana kawaida ya kutumia zaidi ama **mawazo** (mantiki), ama **miguso** (hisi za moyoni), ama **hisi za nje** (milango ya fahamu) ama **machale** (kuona mbali). Hivyo tunapata **aina nane za silika (2x4)**.

Mndani wa mawazo	Mndani wa miguso	Mndani wa hisi za nje	Mndani wa machale
Msondani wa mawazo	Msondani wa miguso	Msondani wa hisi za nje	Msondani wa machale

**A. Wanaotumia mawazo** katika kupima, kuchanganua, kupanga, kuchagua na kuamua mambo wanazingatia **ukweli** wa hakika (sheria na uthibitisho) kuliko msukumo wa moyo na maoni ya wengine. Ni **wachambuzi**: wanajitahidi kuelewa undani wa kila mada, kujuu daima zaidi na kupata maelezo juu ya malengo na matazamio. Wanazingatia matokeo ya tafakuri yao. Wanapenda **utaratibu** na kupanga mambo. Wana **msimamo** kwa kuwa wanajua wanataka nini. Baada ya kuamua anapenda kutekeleza. Wanapima mambo **bila ya kujali utu**, kwa kuwa kwao **sheria na haki** zinashika nafasi ya kwanza; hivyo pengine wanaumiza bila ya kujitambua. Wanaposema wanafuata mawazo yao, wanaeleza vizuri habari pamoja na rai zao na ni hodari kutoa hoja. Si welesi kuonyesha wanavyohisi moyoni. Ajenda zao binafsi ni muhimu kwao. Hawana muda mwingi kwa mahitaji ya wengine. **Hawana upendeleo**, nao wenyewe wanataka kutendewa kwa haki. Wanaona vigumu kusifu na kupongeza, bali wako radhi **kukosoa**, kukemea na kushambulia wengine. Wanajihuisha na haki (stahili za watu) hata kuleta mapinduzi nichini. **Wanafaa kuongoza** (utawala na utekelezaji). Katika migongano wanajitafutia usalama. Katika michezo wanataka ushindi. Wanajiuliza, "Nitumie njia gani? Nipangeje mawazo yangu vizuri?"

**B. Wanaotumia miguso** wanazingatia **hasa utu**. Wanapokusanya maarifa wanapatwa na maono kuhusiana nayo. Wanaamua kufuatana na tunu zao. Mara nydingi wanaacha uamuvi uchukuliwa na wengine ("unichagulie"). Wanatawaliwa na hisi za moyo kuliko kufuata fikra na hoja. Wanajali na **kushiriki miguso ya wengine**. Wanapenda kuwafurahisha hata katika mambo yasiyo na maana. Ni hodari kushughulikia hali yao na hawapendi kuwaudhi: hivyo wanakimbilia masengenyo. Ni **wapendevu**, watulivu, welesi kusamehe. Wanajitahidi kukwepa migongano na kutatua matatizo. Wanapendekeza umoja na hisia nzuri. Wanapenda kuthaminiwa na **kupongezwa**, hivyo hawana raha ikiwa wengine hawawayali, hawawaamini wala kuwakumbuka. Wanaelekeea kusikitika na kuumia. Wako macho kuorodhesha wanaojitolea na kuchangia ustawi wa jamii, na kushauri kuhusu masuala hayo. Wanaposema wanatumia mifano, hadithi na mang'amuzi yao. Wanajiuliza, "Nani ataguswa na uamuvi wangu?"

**C. Wanaotumia hisi za nje** katika kutambua hali halisi na utendaji ambao unahitajika na kuwezekana. Kwa kawaida ni **hodari kuamua** mambo na kutenda kadiri ya mazingira bila ya kusitasita. Kisha kuamua wanataka kutekeleza mara moja, wasiwe na raha mpaka uamuvi wao utimizwe. Ni hodari kwa kazi fupi. Hawapendi kuwaza hewani. Wanaamini **mang'amuzi** kuliko miguso. Kwao ni vigumu kujinyima matakwa ya milango ya fahamu. Wanapenda mno **starehe** na anasa, wanafuata tamaa za mwili. Wanathamini sana maoni na **kusema ukweli**. Hawaogopi kukabili wengine. Katika maelezo yao wanatumia maneno mengi na kufuata utaratibu. Wanajiuliza, "Hali ni ipi? Nifanye nini?"

**D. Wanaotumia machale** katika kutambua mambo wanapendelea yale ya kutarajiwa (hata kama ni ndoto za mchana) kuliko yaliyopo sasa hivi. Wanapendelea mambo **magumu na yasiyojulikana**, hata yakiwa juu ya uwezo wao. Wanapenda kuvumbua vyote vinavyowezekana na **kutabiri** yatakayotokea (faida, hasara n.k.). Wanapenda mawazo ghafla na kama kwa kuota. Wana **matazamio makubwa**, tena wanapenda kuvuka malengo, lakini kabla hawajayafikia, wanayarukia mengine. Hivyo wanafanya **mambo mbalimbali kwa wakati mmoja**. Hawapendi kufanya yaleyale daima, bali kufanya au kujifunza mapya. Ni hodari kuzua mambo, kuanzisha, kuleta **mabadiliko katika yote**. Wanawenza kuhamasisha watu ili nao wapate mawazo mapya na kuona mambo yanayowezekana. Hawaridhiki na ukweli unaoleweka, wanatafuta ule uliofichika au sababu zake ("huyu ni hivi kwa sababu..."). Wanapendelea kutumia hadhiti, ndoto, mithali, mifano, **mafumbo**, vitendawili, maono, alama n.k. kuliko kusema kwa hakika na wazi. Ni kama wanatafuta njia ya kujieleza. Wanapepesa macho huku na huku **wagundue lolote**. Mitazamo yao juu ya watu na mambo ni ya jumla, hivyo mara nydingi

**wanashindwa kupata picha kamili** kwa kugundua kasoro au sifa ndogondogo. Hawawezi kuongoza. Wakifanya kazi wanaifanya kwa bidii hasa. Wanajiuliza, "Mambo gani yanawezekana katika maisha yangu?"

## UMUHIMU WA KUWA NA SILIKA MCHANGANYIKO

Kila silika ina sifa na kasoro. Tunahitaji kufikia **uwiano** fulani ndani mwetu kwa kujifunza toka kwa wenzetu, na hasa kwa Yesu aliye kielelezo kwa wote. Vilevile katika jamii **silika tofauti zinatakiwa kukamilishana**. Hivyo **mtu wa mawazo anamhitaji anayefuata miguso** ili kutabiri miguso ya wengine (watajisikiaje), kubembeleza, kupatanisha, kushawishi, kutangaza mambo, kuuza, kusadikisha na kuamsha shauku na bidii. Upande wake, **anayetumia miguso anamhitaji mtu wa mawazo** ili kuchanganua, kutofautisha, kupanga, kupima matukio, kufuata sheria na mwongozo, kutambua makosa kabla ya kutenda, kutambua kasoro zilizopo ili kusonga mbele, kutaarifu yanayotakiwa kuarifiwa, kuwa imara mbele ya upinzani, kuongoza kwa msimamo, kufukuza watu kazini kama ni lazima.

Vilevile **anayefuata hisi za nje anamhitaji mtu wa machale** ili kusoma alama za nyakati zijazo, kuona namna ya kujianaa kwa kesho, kuangalia mahitaji mapya, kukabili magumu kwa bidii kuleta uwezekano mpya, kuwa na shauku, kutambua heri ijayo ilivyo tumaini letu halisi. Upande wake, **mtu wa machale anamhitaji mtu anayefuata hisi** ili kuangalia kila kitu, kusoma mawazo ya wengine, kuzingatia masharti yote ya mkataba, kujua kinachohitajika sasa hivi, kuzingatia tunaishi leo si kesho, hivyo furaha ya sasa ni muhimu, kutunza kumbukumbu, kukabili matatizo, kusubiri na hatimaye kuleta matokeo ya kufaa.

Kumbe mara nyangi tunapuuuzia mtazamo na vipawa vya wengine; matokeo yake tunaishi na kufanya kazi kwa kukwaruzana. Sababu ya kwanza ni **kutojielewa wala kuelewa watu** na maeleko yao. Basi, silika moja ikitaka kutawala bila ya kujali wengine, inajitafutia hoja hata za kidini, kumbe ni **suala la saikolojia tu:** k.mf. kuhusu kuacha mlango wazi kwa wageni au kuufunga.

## UTAMBUZI WA SILIKA KWA NJIA YA MWANDIKO

Wataalamu wengine hawakubali aina hizo za upambanuzi wa silika, wakidai zinalinganisha watu bila ya kujali tofauti nyangi zilizopo kati ya kila mmoja na wengine wote. Hao wanasisitiza kuwa **watu ni mbalimbali kama alama za vidole vyao**, yaani silika ya kila mtu ni ya pekee. Kazi yetu ni kuitambua kinaganaga, badala ya kuilazimisha ndani ya fremu fulani. Mwenendo mzima wa mtu, hasa asipotenda kwa makusudi, **unamtambulisha** (k.mf. mwendo wake wa kasi au wa taratibu, wa kelele au wa kimyakimya, n.k.).

Tangu zามani sana, watu kadhaa wa China, India, Ugiriki na Italia walivutiwa na jinsi mwandiko wa kila mmoja ulivyo tofauti na ule wa wengine, wakaona unadokeza nafsi yake. Kuanzia karne XVII vilianza kutungwa vitabu kuhusu suala hilo, mpaka ikakubalika **sayansi ya mwandiko** (grafolojia) inayochunguza uhusiano kati ya mwandiko wa mtu na undani na nafsi yake (akili, maeleko, vipawa, umbo, maradhi n.k.). Msingi wake ni kwamba **hatuandiki kwa mkono tu**, kwa kuwa huo unaongozwa na ubongo. Mtu anapoacha kuiga herufi alizofundishwa kwa kuwa amezoea kuandika, anakuja **kutokeza nafsi** yake mwenyewe katika upekee wake. Tunaweza kusema mtu anapoandika bila ya kuzingatia usanifu wa herufi **anajichora** jinsi alivyo.

Wataalamu wa fani hiyo wanazingatia hasa kama mwandiko ni wa mviringomviringo au una pembe na ncha, unakandamiza karatasi kwa nguvu au la, ni mkubwa au mdogo, ni mpana au mwembamba, unapendeza kwa ulinganifu wa herufi zake au la, unafanyika kwa kasi au polepole, unakwenda wima ingawa karatasi haina mstari au huenda ukapanda ama kushuka, unaelekea upande gani, una mapambo au la, n.k. **Kila sifa** ya mwandiko ina sababu yake na hivyo kudokeza silika ya mtu upande wa akili, utashi n.k. Lakini baada ya kuzizingatia zote ni muhimu **kuziona zote kwa pamoja** ili kumtambua mtu mzima jinsi alivyo, na hatimaye kumsaidia maishani.

## KUJUA UKWELI KUHUSU UWEZO WA KUZAA

Wavulana wanaongelea **siri** zao wasitake wasichana wazijue, na wasichana wanafanya vilevile **kati yao**. Zamani ilikuwa kawaida kwetu waziongelee na **wazee** (babu, bibi, n.k.). Mara nyangi kwa njia hizo zilienea **habari zisizoaminika**, kwa kuwa waliota maelezo hawakuwa na ujuzi wa sayansi, tena pengine mtazamo wa maadili ulikuwa mpungufu. Siku hizi **tunaweza tukapotoshwa** zaidi, tena kwa makusudi, na vipindi shulenii na vyombo vya upashanaji habari vinavyopiga vita msimamo sahihi wa Kanisa hasa upande wa jinsia na uzazi, **vikipuuzia usafi wa moyo na hata uhai wa watoto**. Mkazo ni kwamba tuzini tu, mradi tukwepe matokeo yake, yaani mimba na maradhi. Hivyo watu wanaelekezwa wazidi kuzama katika **machafu badala ya kulenga ukomavu** na uadilifu kwa bidii zote na kwa kujiombea msaada wa neema ya Mungu.

Wanaelekezwa kufuata anasa kwa kukwepa uzazi wasije wakaongezeka wakalazimika kujitafutia **mahitaji halisi** (chakula, matibabu, mavazi n.k.) badala ya ziada zinazoleta faida kubwa kwa wafanyabiashara matajiri (soda, tumbaku, simu n.k.). Katika kulenga **anasa bila ya kuwajibika** (kwa watoto watarajiwa) wanaelekezwa na propaganda wazitumie njia za **teknolojia** za kupanga uzazi ambazo (tofauti na njia halali zinazotegemea maumbile) zina gharama kwa watumiaji na hivyo **faida kwa watengenezaji**. Vilevile wanahamasishwa kuharibu mimba, ambazo pia ni chanzo cha mapato makubwa kwa wale wanaoziuwa na kwa wale wanaozitumia katika maabara zao kwa **majaribio na utengenezaji wa dawa** na vipodozi.

Hasa katika hali hiyo ni rahisi kuona umuhimu wa **kujuu mapema ukweli** kuhusu umbile zima la binadamu. Kadiri mtoto anavyozidi kukua anahitaji **kujifahamu kijinsia** aweze kukomaa na hatimaye kuzaa kadiri ya mpango wa Mungu. Ndiyo sababu Kanisa linataka mafundisho hayo yatolewe kuanzia utoto na kukamilishwa kabla mtu hajachagua maisha (njia ya ndoa au nyininge) ili aweze kujua anafanya nini au anaacha nini.

Shida ni kukubaliana kuhusu ufundishaji: k.mf. **nani ana haki na wajibu** wa kuamua mafundisho yatolewe vi? Kwa kuwa **watoto ni wa wazazi hasa**, uamuzi ni juu yao na juu ya viongozi wa dini yao. Serikali inaweza tu kuwasaidia katika kazi hiyo mradi isiiingilie maadili yao.

## UTAKATIFU WA UHAI NA JINSIA

Katika mila nzuri za Mwafrika mojawapo inafundisha kuheshimu viungo vya uzazi kama **milango ya uhai**. Kwake **uhai ni jambo takatifu** linalotokana na Mungu ambalo binadamu anapaswa kulistawisha kwa kila namna upande wake binafsi na upande wa jamii (ukoo n.k.). Kwa msingi huo kila kitu **kinachohusu uzazi kinaheshimika**. Mtazamo huo unakwenda kinyume cha ule unaoenea sasa kuanzia nchi za magharibi, ambaa unaona mwili na jinsia kuwa ni vyombo vya kuchezea tu ili kujifurahisha bila ya kuwajibika kwa ustawi wa uhai.

Utakatifu wa uhai na jinsia unatokana na ukweli kwamba mtu kwa mpango wa Mungu anaweza **kushiriki katika uumbaji wa wengine ambaao waishi milele**. Ukweli huo unaelewaka kwa akili yetu tena umefunuliwa na Mungu. Upande mmoja yeye haumbi binadamu pasipo wazazi; upande mwengine wazazi wakiungana na kuwezesha mimba ipatikane, mara tu **Mungu anaitia roho**. Hivyo imani yetu inaiunga mkono mila ya kuheshimu milango ya uhai kama fumbo la ajabu. Kuliheshimu hakutuondolei wajibu na haki ya kulichunguza kwa njia ya **sayansi** ili tufurahie maajabu ya Mungu, halafu tuelewe na kutekeleza vizuri zaidi **mpango wake**. Hivyo tunaipokea kwa mikono miwili zawadi hiyo kubwa na kuifanyia kazi ili **kumpendeza aliyetuzawadia**; si kuitupa kama kitu cha bure wala kuitumia kwa madhara.

Tunapaswa kuelewa:

1. jinsi tulivyoumbwa kama **umoja wa roho na mwili**;
2. tena tulivyoumbwa **wanaume au wanawake toka kichwa hadi kidole** cha mguu: **jinsia si viungo vya uzazi tu**:
3. viungo yetu hivyo jinsi vilivyo na vinavyofanya kazi;
4. jinsi kazi hiyo inavyoelekea **muungano** na mtu wa jinsia nyininge na kwa njia hiyo **uzazi** pia.

Ndipo tutakapoweza **kuwajibika katika ndoa au kujinyima** kwa lengo lingine kubwa zaidi.

## MABADILIKO YA UBALEHE

Ingawa kila mmojawetu ni mwanamume au mwanamke tangu atungwe, kabla ya **kubalehe** hatuonekani kutofautiana sana, isipokuwa katika viungo vya uzazi. Kumbe muda unafika wa watoto kuanza kukomaa kijinsia: ndipo tofauti zinapoitokeza wazi.

Kutoka utotoni kuingia utu uzima kuna **mabadiliko ya haraka** katika viungo, hisia na roho. Kama ilivyo kwa viumbe hai wote, ustawi huo unaweza ukawahi au kucheleva, lakini kwa kawaida unatokea kati ya umri wa **miaka 12 na 16**. Wasichana wanawahi kuliko wavulana, na Wazungu kuliko Waafrika, lakini mabadiliko ni yaleyale, nayo yanafanyika hatua kwa hatua. Katika hayo, **mengine yanamfurahisha** kijana, lakini mengine hayampendezi, **anayonea aibu** hata kuyafadhaikia hasa asipoyaelewa. Bila ya shaka **anahitaji msaada** wa walezi aweze kukabili hayo yote bila ya kuvurugika kiasi cha kupotoka.

Kwanza mvulana anajikuta **akirefuka haraka** na kupata misuli mikubwa; kifua kinapanuka. Papo hapo **sauti** yake inaanza kupasuka na kuwa nzito, ndeuu zinawenza zikaota, na vilevile **malaika** sehemu za siri, kwapani na pengine kifuanu. Hali ya **ngozi** inakuwa ikikwaruzakwaruza hasa usoni, na chunusi hujitokeza. Katika hatua ya mbele mabadiliko yanahusu zaidi **viungo vya uzazi** vinavyokua na kuanza kazi ambayo kwa kawaida **kwa mvulana itaendelea moja kwa moja**, kumbe **kwa msichana itakoma kati ya miaka 40 na 50**. Huyo vilevile anabadilika ili kuijandaa kuwa mama. Mwili unastawisha **maziwa, ukubwa na uzuri** wa umbo, malaika sehemu za siri na kwapani, mabadiliko ya **rangi** ya uso. Hatimaye anavunja ungo, yaani anaanza kutokwa na damu katika tumbo la uzazi. Kwa kawaida itatokea **mara moja kwa mwezi**, lakini itawenza ikawahi au kucheleva kutokana na hali yake ya mwili na ya nafsi (shughuli nyangi, mahangaiko, uhamisho n.k.). Sababu ya damu kutoka ni kwamba, kijiyai kilichokomaa na kutoka nje ya kifuko cha vijiyai kisipopata mbegu ya mwanamume baada ya siku moja **kinaharibika harakaharaka**; hapo ngozi nyembamba ya tumbo la uzazi, iliyotanuka kwa damu ili kupokea na kulisha mimba, **inachanikachanika** na kutoa damu. Kumbe mbegu ikikifikia kijiyai, **mimba inapatikana** na kujishikiza kwenye kuta za tumbo la uzazi ili iendelee kukua; hapo damu haitoki na mama anaweza kujihisi mjaa mzito.

Mabadiliko ya mwili yanaendana na **mengine ya nafsi** yanayofanya tabia iwe tofauti na ile ya awali. **Hisia zinabadiika** kadiri mwili unavyozidi kutengeneza chachu (**homoni**) zinazomfanya kijana aelekee namna ya baba au mama zake. Mvulana anajikuta akivutiwa na uzuri wa wasichana, na kupenda kuwajua zaidi, kuongea nao n.k. Anapenda **kuwagombeza** na kuwaonea ili aonyeshe uwezo na nguvu alivyonavyo. Katika hatua hiyo anakuwa **mvivu na mzito** katika kutembea na mara nydingi **hajali unadhifu**. Kumbe msichana anazidi kupenda sifa na **kujiremba**.

**Akili pia inapevuka** na kumfanya kijana apende kuwa na maoni maalumu kuhusu mambo mbalimbali, hata kubishana na wengine. Pia apende **mabadiliko, ujuzi mpya** n.k. Ndiyo sababu kijana **si mwepesi kupokea mashauri** na maoni ya wakubwa, asije akajisikia tena mtoto huku akipenda **kutambulika amekuwa mtu mzima**. Kwa ajili hiyo anatamani kufanya yale wanayoyafanya wakubwa (kuvuta sigara, kurudi nyumbani usiku n.k.), kushirikiana na **rika** lake na hata kujiunga na **makundi** ya wanaomzidi katika shughuli zao (magenge, timu n.k.) ingawa pengine hazifai (uhuni, bangi n.k.).

Hatimaye kuna **mabadiliko upande wa roho**: kati ya mawazo mengine, kijana anajitafutia **msimamo mpya** kuhusu maswali makuu ya maisha: anataka kuwa na falsafa na dini yake. Shida ni kwamba usahihi wa majibu unategemea sana uadilifu wa maisha: kijana **akifuata anasa, akili inapofuka** na imani inapotea.

## VIUNGO VYA UZAZI

**Uume (mboo)** wa mvulana unakua, lakini kwa **kiasi tofauti** kati ya mtu na mtu. Kila mmoja **ajipokee** alivyo hata katika kiungo hicho, bila ya kuhangaika wala kuona aibu kwa sababu, eti ni kidogo. **Tohara ni upasuaaji mdogo** wa kukata na kuondoa govi, yaani ngozi inayofunika kichwa cha uume. Inaweza kufanyika katika **umri wowote** na kwa **sababu mbalimbali**. Kwa Wayahudi ni ishara ya agano lao na Mungu na inapaswa kufanyika siku ya nane baada ya kuzaliwa ili kumuingiza mapema katika taifa la Mungu. Katika makabila mengi ya Afrika mvulana anatahiriwa ili kuingizwa katika kundi la wanaume wanaopaswa kuwajibika katika jamii. Siku hizi hata mataifa yasiyokuwa na desturi hiyo yanaanza kujiali kwa sababu za **usafi na afya**. Tofauti kabisa ni **ukeketaji** unaowaondolea wanawake sehemu ndogo au kubwa ya viungo vya uzazi kusudi wasifurahie sana tendo la ndoa, hivyo wawe waaminifu zaidi kwa waume wao. Hiyo ni **mila mbaya** inayosababisha wasichana wengi kufa na wengine wengi kupatwa na maumivu makali wakati wa hedhi, wa tendo la ndoa na wa kujifungua.

**Kusimika** kwa uume si jambo jipya kwa kuwa utotoni limeshatokea kawaida kutokana na kibofu kujaa mkojo. Ila sasa linaweza kutokea **kwa sababu mpya**, yaani jinsia. Muundo wa uume ni **misuli aina ya sifongo** yenyne neva nyangi. Kukiwa na msisimko **damu inajaa** nafasi zilizomo na kusababisha uume **utanuke na kusimama** imara na wima. Kusimika kunajitokeza na kupotea haraka kutegemeana na hali iliyopo. Hali hiyo inaweza kutokea bila ya mtu kutaka, kwa mfano usiku au pia mchana kati ya watu ikimfanya aone haya. Upande wa maadili tuisababishe hali hiyo bila ya **lengo jema**, kama vile kumtibu mgonjwa, kuungamisha au kujielimisha kuhusu jinsia. Kwa hiyo **tukwepe** kwa kawaida yale yote yanayoweza kusisimua, kama vile mawazo, maneno, masomo, mitazamo na vitendo mbalimbali kuhusu jinsia. Mvulana anahitaji kujifunza nidhamu ya namna hiyo. Mashauri mengine ni kutovaa kaptura wala suruali zinazobana, na kuficha kwa adabu hali hiyo ikitokea, lakini **bila ya kuiogopa** wala kudhani ni dhambi.

**Mapumbu** yanaanza kutengeneza **mbegu za kibinadamu** kwa wingi sana: hizo ni **ndogondogo** na zina umbo kama la viluwiluvi vya chura, yaani vina **vichwa na mikia tu**. Vichwa ndivyo vinavyoleta **viini vya urithi** wa baba. Mikia kazi yake ni kusaidia tu **kusukuma mbegu** ndani ya tumbo la uzazi mpaka zikutane na kijiyai cha mama, halafu inapotea ndani ya kijiyai. Mbegu zikiwa tayari **zinahifadhiwa** kwanza katika kifuko cha akiba, karibu na kibofu, zikisubiri msisimko wa kijinsia ili **zitoke kwa njia ya uume** na kuanza mashindano ya **kutafuta kijiyai**, zikisaidiwa na majimaji ambayo yanaitwa **shahawa** na kutengenezwa ndani ya kifuko. Shahawa inafuata mshipa wa mkojo bila ya kuchanganyikana nao.

Shahawa inaweza ikatoka hata nje ya **tumbo la uzazi la mke, lililo shabaha yake**, kwa kuwa inalenga uzazi hasa. Inaweza ikatokea k.mf. kutokana na **ndoto za usiku**, bila ya mtu kukusudia; huyo anaweza akazinduka mara au kutambua asubuhi tu kilichotokea. Kwa vyovyote **asihangaike** kwa kuwa hilo ni jambo la kawaida **lililopangwa na Mungu** ili kumsaidia mwanamume **asiye na mwenzi**. Maana mbegu zake kadiri zinavyoongezeka katika kifuko cha akiba zinataka kutoka, hivyo zinamuelekeza kwenye matendo ya kijinsia. Basi, kwa ndoto hizo mbegu zinapungua bila ya dhambi, na **vishawishi vinakosa ukali** wake. Ni suala la kusubiri tu na kuwa na hakika kwamba havitadumu muda mrefu kwa nguvu ileile. Upande wa wasichana pia, kuna siku zenye mvuto mkubwa wa kijinsia, kuhusiana na mabadiliko ya kila mwezi yanayoendana na kijiyai kukomaa; **inatosha kusubiri** nao utapungua mapema.

Mvulana anapotokwa na shahawa kwa mara ya kwanza ni dalili ya kuwa **si mtoto tena**, bali ana **uwezo wa kuzaa**: kwa hiyo **awajibike** kama mtu mzima kuhusu uwezo mpya aliojaliwa. Hasa azingatie kuwa uwezo wake huo **bado ni mbichi**: ingawa unaweza kusababisha mimba, mimba hiyo itaendelea kwa shida au kufa kabisa. Ubichi ni mkubwa **zaidi upande wa nafsi**, kwa kuwa mvulana hajawa tayari kubeba mzigo wa familia mpya. Ndiyo sababu asichezee uwezo huo, bali **ajiandae kuwa baba safi** siku za mbele: ajipatie elimu au ufundi fulani, akomae kiutu na kutunza afya yake ya mwili na ya nafsi. Msichana afanye vilevile aweze kuwa mama bora; kumbe akijiingiza mapema katika masuala ya ngono, **anahatarisha heshima yake pamoja na afya**, kwa kuambukizwa maradhi yanayoweza yakasababisha utasa au kwa kuzaa kwa shida kabla ya wakati wa kufaa.

## MKAMILISHANO NA UZAZI

Jinsia **zinalenga kukamilishana** katika ndoa. Mungu baada ya kumuumba Adamu alisema, "Si vema mtu awe peke yake. Nitamfanyia msaidizi wa kufanana naye" (Mwa 2:18). Umbile la mwanamume linaelekeea

kukamilishana na lile la mwanamke **kiroho na kimwili**. Lakini roho haionekani, hivyo ni rahisi zaidi kuona jinsi **miili yao inavyofaa kuungana** iwe mwili mmoja. Hata hivyo tuelewe mkamilishano huo unafanyika katika nafsi pia, ambazo zina **vipaji tofauti** vinavyowezesha kwa pamoja **kukabili vizuri maisha** ya nyumbani, ya uchumi, ya siasa, ya dini n.k.

Tukiangalia viungo vya uzazi nya kike tunakuta kwenye kilango chake **kizinda**, yaani nyama nyembamba inayoondolewa na mwanamume wa kwanza anayekiingilia. Ndiyo sababu ni kama **mhuri wa ubikira** wa mwanamke. Katikati ya kizinda kuna tundu dogo tu kupitishia damu wakati wa **hedhi**, yaani siku zile ambazo anatokwa damu kupitia **uke** ulio nafasi ya wazi (kati ya kizinda na tumbo la uzazi) iliyo tayari kupokea uume na mbegu zake. Hizo **zinasafiri** muda wa **saa sita** hivi **katika tumbo la uzazi** ili kukifiki kijiyai katika **mrija** unaoliunganisha na kifuko cha kijiyai. Mbegu zinazofunga safari hiyo zinaweza kuwa **milioni kadhaa**, lakini chache tu zitafika; tena kati yake, **moja tu itapenya kijiyai**, kwa sababu mara tu inapoingia kijiyaji kinakuwa kigumu kwa nje, hivi kwamba mbegu nyininge zitagonga bure. Ikiwa mbegu hiyo inabeba **kromosomu Y** mtoto atakuwa wa kiume, la sivo atakuwa wa kike.

Mbegu na kijiyai vinapounganika, **viini nya urithi** vinavyobebwa navyo **vinachanganyikana** kwa namna mojawapo kati ya zile zote zinazowezekana. Kwa kawaida viini hivyo ni **46 kwa kila mtu**, na kila seli ya mwili wake inavyo. Katika viini hivyo zimo **jeni 25,000** hivi, yaani sifa zote za mtu huyo maalumu tangu atungwe hadi afe. Viini hivyo vinaongoza ujenzi wa mwili kwanza tumboni mwa mama, halafu utengenezaji wa seli mpya baada ya kuzaliwa. Hata mbegu zote zina viini hivyo nya baba, na vijiyai vyote vina viini hivyo nya mama, isipokuwa katika kukomaa **vinapungua na kubaki 23 tu** kusudi mbegu na kijiyai vikiungana mimba inayopatikana iwe na **viini 46** kama kawaida. Kutokana na **wingi usiohesabika** wa namna ambazo jeni hizo zinaweza kuchanganyikana, **hakuna mtu aliye sawa na mwingine**, kama vile alama za vidole zilivyo tofautifauti. Hivyo toka mwanzo mimba hiyo ni **mtu wa pekee**, ingawa ina seli moja tu. Seli hiyo itakua na kuanza **kugawanyika** katika seli 2, 4, 8, 16 n.k. Ingawa kila moja ina viini vilevile, **polepole seli zitafautiana** ili kufanya kazi maalumu (ubongo, moyo na viungo vingine) na kushirikiana zote vizuri katika umoja wa mwili. Baada ya **miezi miwili viungo vyote** vimeshatengenezwa, halafu vinazidi kukua na kukamilika hadi **mwezi wa tisa** ambapo mwishoni mwake mtoto atazaliwa.

## MAOVU

Badala ya kuheshimu kwa shukrani maajabu hayo ya Mungu, mara nydingi binadamu, aliyeshirikishwa naye katika kazi ya kuumba, amejifanya **muuaji wa watoto** wasizaliwa bado na wa wale waliozaliwa pia. Sababu zinaweza kuwa mbalimbali: haya, hali ya uchumi, ulemavu, ubaguzi wa jinsia n.k. Kwa vyovyote **uuaji unamlilia Mungu aliye kisasi**.

Jambo baya zaidi, siku hizi katika nchi nydingi uuaji wa mimba **umehalalishwa** na mabunge na umekuwa ukichangiwa na serikali. Kwa njia hiyo kila mwaka **watoto milioni mia na zaidi wanaangamizwa** kwa ukatili wasizaliwe, bila ya kuhesabu wale wanaouawa na **vidonge, sindano, poda, vitanzi na vipandikizi**, pengine bila ya wahusika kujua wala kutambua kilichotokea. Kwa kuwa hivyo vinatangazwa kama njia za uzazi wa majira unaopanga upatikanaji wa mimba, kumbe ukweli ni kwamba **vinaua mimba** zilizokwishaumbwa, mbali ya kwamba **vinaharibu afya** ya akina mama.

Kwa kawaida mauaji hayo ya halaiki yanaandalila njia na jitihada za **kukwepa mimba kwa mbinu yoyote**, hivi kwamba ikishindikana mtu anafikia uamuzi wa kuua. Baadhi ya njia hizo za kuzuia uzazi ni: **kumwaga mbegu nje ya tumbo la uzazi, mipira ya kiume na ya kike, kufunga kizazi cha mwanamume au cha mwanamke**. Ingawa njia hizo **hazui mimba, zinaleta madhara** kwa wanaozifuata, tena zinashindikana kwa kiasi tofauti.

**Kanisa halikubali hata moja** kati ya mbinu hizo, ila inaelekeza wanaohitaji kuairisha uzazi **watumie ndoa siku zile ambazo mwanamke hawezi kupata mimba** (yaani siku zote isipokuwa **nne kwa mwezi**, au zaidi ikiwa hana mwendo wa kawaida). Njia hiyo ya asili **haina madhara** yoyote, wala **haijengi hofu** na chuki kwa mimba, wala **haina gharama**, hatimaye **ina hakika kubwa** (98-99% katika mtindo wa kupima ute wa uke uliovumbuliwa na bwana na bibi Billings). Njia hiyo inayofuata sayansi bila ya **teknolojia** inadai sadaka ya kujizua kidogo, lakini uwajibikaji wa pamoja wa mume na mke unaohitajika unaweza **kustawisha ushirikiano** na uelewano kati yao. Siku ambazo wanapumzika tendo la ndoa, upendo wao unaweza kujitoneza na kukua kwa **njia tofauti** (maongezi, matembezi na vitendo vidogovidogo nya mapenzi) bila ya kutumia tendo la ndoa tu, kama kwamba ni **dozi** inayohitajika mara kwa mara.

Kinyume chake, njia za teknolojia zinategemea uamuzi hata wa mmojawao tu, zinajenga **ubinafsi**, zinamfanya mwanamume hasa azingatie **kujamiiiana tu** hata mwanamke asiridhike na hivyo asipende kuungana na mumewe tena, zinaelekeza **kutembea nje ya ndoa** bila ya wasiwasi n.k. Kwa hiyo njia hizo zinachangia sana kufanya ndoa **zivunjiwe, watoto watelekezwe na nchi ziharibile**, kama mang'amuza yanavyoonyesha. Bahati mbaya wanaozitegemea kwa kufaidika ni matajiri, nao wako tayari kutumia **pesa nydingi ili kuzieneza** hasa katika nchi maskini (k.mf. serikali ya Marekani na makampuni yake yanatafuta masoko mapya kwa biashara yao baada ya wateja wa nchi tajiri kuanza kung'amua madhara ya vifaa hivyo).

## MARADHI YA ZINAA

Vitendo nya kijinsia ni **njia ya kuambukiza** maradhi mbalimbali, mengine ya zamani (kisonono, kaswende n.k.), na mengine mapya (ukimwi n.k.). Katika hayo pia tunaona kwamba **uzinifu unamdhuru binadamu**: hatuwezi kuchezea utakatifu wa uhai tusipate hasara **kiroho, kijamii na pengine hata kimwili**.

## PUNYETO

**Punyeto ni hatua tofauti** ambayo vijana wengine wanaichukua ili wajipatie kionjo cha kuridhisha kinachofanana na kile cha tendo la ndoa. Kwa kawaida wanaskumwa na msisimko uliowapata, pamoja na haya ya kujitafutia mtu na hofu ya kuambukizwa maradhi. Hata hivyo kufanya hivyo ni **kupotosha maana ya jinsia** katika mpango wa Muumba kwa binadamu, ambao ni kufanya wawili wawe kitu kimoja kwa nguvu ya **upendo ambaao uanze rohoni** na kukamilika katika muungano wa miili yao. Upendo maana yake ni **kujitoa** kwa muungano na mpenzi unoleta **tunda lake katika mtoto**, ambaye ni kwa pamoja wa baba na wa mama, **akiwaunganisha upya** ndani mwake.

Katika tendo la kujichua **hakuna lolote kati ya hayo**: hakuna upendo wala kujitoa kwa wengine, hakuna muungano wala uzazi, isipokuwa kujitafutia iwezekanavyo furaha ya kimwili (**ashiki**) iliyokusudiwa na Mungu kuwa **sehemu ya furaha nzima** ya muungano wa ndoa. Katika tendo hilo la **ubinafsi** mtu yuko peke yake na kubaki peke yake: **halengi chocchote nje ya mwili wake**, hivyo anazidi kuzama ndani mwake badala ya kustawi kwa kuiwekeea malengo mema (k.mf. ndoa, haki, huduma kwa wenye shida, utume n.k.). Matokeo yake ni **kupoteza nguvu za mwili** na hasa **kuvuruga msimamo wa nafsi** kwa kujisikia mnyonge, mwenye kosa na mtumwa wa tendo ambalo analikinai mara tu baada ya kilitenda. Hatimaye anaweza kupata matatizo katika tendo la ndoa.

Kwa msingi huo Kanisa linahesabu punyeto kuwa **dhambi kubwa**, tena upande mmoja ni kubwa kuliko uasherati (kuzini kati ya msichana na mvulana), kwa sababu linakwenda **kinyume cha maumbile** na kuanda njia kwa dhambi nyingine (k.mf. **ushoga**). Hata hivyo elimunafsia inatueleza pia **urahisi kwa mtu asiyekomaa** kimapendo kufuata njia hiyo danganyifu, tena ngumu kuachwa baada ya kuzoleka. Ndiyo sababu Kanisa linamhimiza padri kupokea kwa **huruma** wenye tatizo hilo na kuwasaidia **mashauri ya kibinadamu** pia kuhusu afya ya mwili na ya nafsi. Kwa mfano: kunyosha viungo kwa kazi za mikono au kwa michezo, kulalia pagumu tena siyo kifudifudi, kukwepa vinywaji vinavyochochea neva (kahawa, chai n.k.) na vyakula vitamu fulanifulani (pilipili n.k.), kushirikiana zaidi na watu, kusaidia wenye shida. Upande wa roho awashauri kupata **kitubio na ekaristi** mara nyingi, wakiwahi kabla hawajashindwa na vishawishi. Awatumainishe **wanawenza kushinda**, kwa hiyo wasikate tamaa wala wasiogope mno. Ila wakitaka kufuata wito wa upadri au utawa asiwatie moyo mapema: hasa **wasiingie seminari kuu wala unovisi** kabla hawajatatua tatizo hilo.